JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16

OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO

NOVEMBA, 2014

YALIYOMO

UTANGULIZI ---------- v

SURA YA KWANZA ---------- 1
HALI YA UCHUMI ---------- 1
1.1 Hali ya Uchumi wa Dunia ---------- 1
1.2 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka 2013 ---------- 1
1.3 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa kipindi cha nusu mwaka (Januari – Juni 2014) ---------- 3
1.4 Idadi ya Watu na Pato la Kila mtu ---------- 4
1.5 Mfumuko wa Bei ---------- 4
1.6 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Afrika Mashariki ---------- 5
1.7 Ujazi wa Fedha na Karadha ---------- 6
1.8 Mwenendo wa Viwango vya Riba ---------- 6
1.9 Thamani ya Shilingi ---------- 7
1.10 Sekta ya Nje ---------- 7
1.11 Akiba ya Fedha za Kigeni ---------- 7
1.12 Mapato na Matumizi ya Serikali ---------- 8
1.13 Deni la Taifa ---------- 8
1.14 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla ---------- 9

SURA YA PILI ---------- 10
UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ---------- 10
2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ---------- 10
2.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati ---------- 11
2.2.1 Miundombinu ---------- 11
2.2.2 Kilimo ---------- 33
2.2.3 Viwanda ---------- 36
2.2.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu ---------- 38
2.2.5 Huduma za Utalii, Biashara na Fedha ---------- 38
2.3 Miradi Mingine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi ---------- 40
2.3.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundi ---------- 40
2.3.2 Afya na Ustawi wa Jamii ---------- 43
2.3.3 Mifugo na Uvuvi ---------- 43
2.3.4 Madini ---------- 45
2.3.5 Usafiri wa Anga na Majini ---------- 46
2.3.6 Hali ya Hewa ---------- 49
2.3.7 Maendeleo ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu ---------- 49

2.3.8 Ardhi, Nyumba na Makazi ---------- 50
2.3.9 Katiba Mpya ---------- 50
2.3.10 Vitambulisho vya Taifa---------- 51
2.3.11 Kazi na Vijana ---------- 51
2.3.12 Ushirikiano wa Afrika Mashariki ---------- 52
2.3.13 Sekta Binafsi---------- 52

SURA YA TATU ---------- 54
MIRADI YA KIPAUMBELE 2015/16 ---------- 54
3.1 Utangulizi---------- 54
3.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati---------- 54
3.2.1 Miundombinu---------- 54
3.2.2 Kilimo ---------- 59
3.2.3 Viwanda ---------- 60
3.2.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu---------- 61
3.2.5 Huduma za Utalii, Biashara na Fedha ---------- 62
3.3 Miradi Mingine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi---------- 63
3.3.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundi ---------- 63
3.3.2 Afya na Ustawi na Jamii ---------- 64
3.3.3 Mifugo na Uvuvi---------- 64
3.3.4 Madini ---------- 65
3.3.5 Usafiri wa Anga na Majini ---------- 66
3.3.6 Hali ya Hewa ---------- 66
3.3.7 Ardhi, Nyumba na Makazi ---------- 66
3.3.8 Ushirikiano wa Kikanda ---------- 67
3.3.9 Misitu na Wanyamapori---------- 67
3.3.10 Utawala bora ---------- 67
3.3.11 Vitambulisho vya Taifa---------- 68
3.3.12 Kazi na Vijana ---------- 68
3.3.13 Mazingira---------- 68

SURA YA NNE---------- 69
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16 ---------- 69
4.1 Utangulizi---------- 69
4.2 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16)---------- 69
4.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16 ---------- 69
4.4 Vyanzo vya Mapato ya Ndani ---------- 70
4.5 Vyanzo vya Mapato ya Nje ---------- 70

4.6 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ---------- 70
4.7 Uwekezaji wa Sekta Binafsi ---------- 70

SURA YA TANO ---------- 71
UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MIRADI YA MAENDELEO ---------- 71
5.1 Utangulizi ---------- 71
5.2 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo ---------- 71
5.3 Tathmini ya Miradi ya Maendeleo ---------- 73
5.4 Utekelezaji wa Mpango-kazi ---------- 73
5.5 Utekelezaji wa Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa ---------- 74
5.6 Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo 2015/16 ---------- 75
5.7 Muhtasari wa Ratiba ya Utekelezaji ---------- 76

SURA YA SITA ---------- 78
MKAKATI WA KUKABILIANA NA VIASHIRIA HATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO ---------- 78
6.1 Utangulizi ---------- 78
6.2 Viashiria hatarishi vya Utekelezaji wa Mpango ---------- 78
6.3 Hatua za Kukabiliana na Viashiria Hatarishi vya Utekelezaji wa Mpango ---------- 78

KIAMBATANISHO I ---------- 80
BIG RESULTS NOW PROJECTS AND PROGRAMMES 2013/14 – 2015/16 ---------- 80

KIAMBATANISHO II ---------- 83
MAPENDEKEZO YA MAABARA YA KUBORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA NA UWEKEZAJI, 2015/16 ---------- 83

KIAMBATANISHO III ---------- 87
MAPENDEKEZO YA MAABARA YA KUBORESHA HUDUMA ZA AFYA, 2015/16 ---------- 87

UTANGULIZI

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16 ni ya Mpango wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 -2015/16) ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Lengo kuu la mapendekezo haya ni kuongoza utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa ambao Serikali inakusudia kutekeleza katika mwaka 2015/16. Mpango huo utazingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) vifuatavyo: (i) Miundombinu ya nishati, usafirishaji, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), maji safi na maji taka na umwagiliaji; (ii) Kilimo ikijumuisha mazao ya chakula na biashara, ufugaji, uvuvi na misitu; (iii) Viwanda vinavyotumia malighafi hususan za ndani na kuongeza thamani, viwanda vikubwa vya mbolea na saruji, viwanda vya kanda maalum za kiuchumi, kielektroniki na TEHAMA; (iv) Maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi kwa kutilia mkazo sayansi, teknolojia na ubunifu na kuimarisha mafanikio ya upatikanaji wa huduma za jamii; na (v) Uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2015/16 yanalenga kuimarisha utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16). Msisitizo mkubwa utawekwa katika kuendelea kutekeleza programu na miradi ya kitaifa ya kimkakati ikijumuisha miradi iliyo chini ya utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa na miradi mingine muhimu wa ukuaji wa uchumi. Aidha, mapendekezo haya yanazingatia Malengo ya Milenia 2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini - MKUKUTA II (2011-2015); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2010-2015); na Sera na mikakati ya kisekta.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16 yamepangiliwa katika sura kuu sita. Sura ya kwanza inaeleza

mwenendo wa uchumi kwa kipindi cha mwaka 2013 na robo ya kwanza ya mwaka 2014. Aidha, sura hii inabainisha shabaha na malengo yanayotarajiwa kufikiwa katika kipindi cha mwaka 2015/16. Sura ya pili ni mapitio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2013/14 na robo ya kwanza ya mwaka 2014/15 kwa baadhi ya maeneo. Sura ya tatu, ndiyo kiini cha Mapendekezo ya Mpango na inabainisha maeneo yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2015/16. Sura ya nne ni ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16; na Sura ya tano inaainisha ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo na Sura ya Sita inaelezea Mkakati wa Kukabiliana na Vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango.

SURA YA KWANZA
HALI YA UCHUMI

1.1 Hali ya Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Fedha Duniani (IMF-WEO) ya Oktoba, 2014 mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa Dunia kwa mwaka 2014 na 2015 unatarajiwa kuimarika kutokana na kuzingatia kanuni za utekelezaji wa Sera za fedha na bajeti. Pato la Dunia linatarajiwa kukua kwa asilimia 3.3 mwaka 2014 na asilimia 3.8 mwaka 2015 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2013. Ukuaji kwa Nchi Zinazoibukia Kimaendeleo na Zinazoendelea unakisiwa kuwa asilimia 4.4 mwaka 2014 na asilimia 5.0 mwaka 2015. Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa Pato unatarajiwa kuwa asilimia 5.1 mwaka 2014 na asilimia 5.8 mwaka 2015. Kwa upande wa nchi zilizoendelea, ukuaji unatarajiwa kuwa asilimia 1.8 mwaka 2014 na asilimia 2.3 mwaka 2015.

Jedwali Na. 1: Ukuaji wa Pato la Dunia na Matarajio (2008 hadi 2015) (Asilimia)

	Halisi						Matarajio	
	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015
Dunia	2.8	-0.7	5.2	3.9	3.4	3.3	3.3	3.8
Nchi Zilizoendelea	0.1	-3.7	3.2	1.6	1.2	1.4	1.8	2.3
Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea	6.0	2.8	7.3	6.3	5.1	4.7	4.4	5.0
Nchi zinazoibukia Barani Asia	7.7	7.2	9.5	8.0	6.7	6.6	6.5	6.6
Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara	5.6	2.8	5.3	5.3	4.4	5.1	5.1	5.8
Tanzania	7.4	6.0	7.0	6.4	6.9	7.0	7.2	7.4
Kenya	1.5	2.7	5.8	4.4	4.6	5.6	6.3	6.3
Uganda	10.4	4.1	6.2	6.2	2.8	6.0	6.4	6.8
Rwanda	11.2	6.2	7.2	8.2	8.0	5.0	7.5	7.5
Burundi	4.9	3.8	5.1	4.2	4.0	4.5	4.7	4.8

Chanzo: IMF, WEO, Oktoba 2014

1.2 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Mwaka 2013

Pato halisi la Taifa katika mwaka 2013 lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9 mwaka 2012. Shughuli ndogo (sub-activity) ambazo zilikua kwa kasi kubwa katika mwaka 2013 ikilinganishwa na mwaka 2012 ni pamoja na mawasiliano asilimia 22.8;

ujenzi asilimia 8.6; biashara ya jumla na rejareja asilimia 8.3; na hoteli na migahawa asilimia 6.3. Kwa upande mwingine, Ukuaji wa sekta ya Kilimo ulibakia kama ilivyokuwa mwaka 2012 asilimia 4.3 kutokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli ndogo za mazao kutoka asilimia 4.7 mwaka 2012 hadi asilimia 4.5 mwaka 2013 na kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa sekta ndogo ya mifugo na uwindaji asilimia 3.1 hadi asilimia 3.8 na misitu asilimia 2.4 hadi asilimia 3.3. Aidha, shughuli nyingine ndogo ambazo kasi ya ukuaji wake ilipungua katika mwaka 2013 ikilinganishwa na 2012 ni bidhaa za viwandani asilimia 8.2 hadi asilimia 7.7; umeme na gesi asilimia 6.0 hadi asilimia 4.4; uchukuzi asilimia 7.1 hadi asilimia 6.2; na uvuvi asilimia 2.9 hadi asilimia 2.2. **Jedwali Na. 2** linaonesha ukuaji wa shughuli za kiuchumi kwa mwaka 2008 hadi 2013.

Jedwali Na.2: Ukuaji wa Hali wa Pato la Taifa kwa Mwaka 2008-2013

SEKTA	Asilimia					
	2008	2009	2010	2011	2012	2013
Kilimo, Uwindaji na Misitu	**4.6**	**3.2**	**4.2**	**3.6**	**4.3**	**4.3**
Mazao	5.1	3.4	4.4	3.5	4.7	4.5
Mifugo	2.6	2.3	3.4	3.9	3.1	3.8
Uwindaji na Misitu	3.4	3.5	4.1	3.5	2.4	3.3
Uvuvi	**5.0**	**2.7**	**1.5**	**1.2**	**2.9**	**2.2**
Viwanda na Ujenzi	**8.6**	**7.0**	**8.2**	**6.9**	**7.8**	**7.5**
Uchimbaji Madini na Mawe	2.5	1.2	2.7	2.2	7.8	6.9
Bidhaa za Viwandani	9.9	8.0	7.9	7.8	8.2	7.7
Umeme na Gesi	5.4	8.4	10.2	1.5	6.0	4.4
Maji	6.6	5.6	6.3	4.0	5.4	4.9
Ujenzi	10.5	7.5	10.2	9.0	7.8	8.6
Huduma	**8.5**	**7.2**	**8.2**	**7.9**	**8.0**	**8.2**
Uuzaji wa Jumla, Reja reja na Matengenezo	10.0	7.5	8.2	8.1	7.7	8.3
Mahoteli	4.5	4.4	6.1	4.6	4.8	6.3
Uchukuzi	6.9	6.0	7.0	6.7	7.1	6.2
Mawasiliano	20.5	21.9	22.1	19.0	20.6	22.8
Fedha	11.9	9.0	10.1	10.7	13.2	12.2
Upangishaji Majengo na Huduma za Biashara	7.1	6.8	7.0	6.5	6.7	6.4
Utawala	7.0	4.4	6.5	6.8	5.8	5.1
Elimu	6.9	7.1	7.3	7.4	6.5	5.9
Afya	9.0	6.7	6.9	5.4	5.6	5.6
Huduma nyinginezo	3.1	3.2	3.5	3.0	3.8	4.2
Pato la Taifa	**7.4**	**6.0**	**7.1**	**6.4**	**6.9**	**7.0**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2014

1.3 Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Januari – Juni 2014)

Katika nusu ya kwanza (Januari – Juni) ya mwaka 2014, Ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei ya soko uliongezeka kwa kasi ya asilimia 7.1 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2013, (**Kielelezo Namba 1**). Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa viwango vikubwa ni pamoja na uchukuzi na mawasiliano asilimia 16.7, huduma za fedha asilimia 13.6, uzalishaji nishati ya umeme asilimia 10.1 na uzalishaji bidhaa viwandani asilimia 7.7 na biashara za jumla na rejareja asilimia 7.4. Sababu zilizochangia ukuaji katika shughuli hizo ni pamoja na kuwepo kwa hali ya hewa nzuri kwa ajili ya uzalishaji, uwekezaji mkubwa wa miundombinu katika shughuli za uchukuzi na mawasiliano na kuongezeka uzalishaji wa umeme utokanao na mafuta na gesi ulichochea uzalishaji viwandani.

Kielelezo Na 1: Kasi ya Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Kipindi cha Nusu Mwaka (Januari - Juni) 2005 – 2014



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2014

Jedwali Na 3: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Mwaka 2005-2014 katika kipindi cha Nusu Mwaka

Shughuli za Kiuchumi	2005	2006	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014
Kilimo	3.5	5.4	3.6	5.4	1.6	2.6	3.2	3.4	3.7	4.1
Uvuvi	14.8	3.5	2.9	-4.4	9.5	5.2	1.1	4.5	2.2	2.3
Uchimbaji Madini na Mawe	5.3	18.8	13.5	6.4	-23.4	24.0	3.4	7.8	2.1	5.8
Bidhaa za Viwandani	10.8	12.2	7.3	6.1	8.3	6.0	6.6	6.6	7.4	7.7
Umeme	8.5	2.3	11.0	0.2	9.3	7.1	7.4	1.8	5.6	10.1
Ujenzi	0.2	17.5	2.2	3.3	3.7	15.3	2.5	4.0	9.8	6.3
Uuzaji wa Jumla, Reja reja na Matengenezo	6.1	12.1	9.9	11.2	7.9	9.3	9.4	9.6	8.4	7.6
Mahoteli	4.3	1.7	4.0	4.0	3.4	5.3	2.9	3.3	4.5	3.5
Mawasiliano na Uchukuzi	11.3	14.2	-3.7	11.0	9.4	10.8	16.5	14.9	15.6	16.7
Fedha	8.8	11.2	-7.0	15.2	14.5	12.6	10.0	11.8	13.6	13.6
Upangishaji Majengo na Huduma za Biashara	7.6	9.7	8.8	7.7	7.7	9.5	7.7	7.6	7.1	7.4
Utawala	12.7	7.3	6.5	7.4	4.3	6.8	6.1	6.5	4.8	5.0
Elimu	3.7	6.1	5.8	5.4	7.3	6.5	5.5	6.3	6.4	5.8
Huduma Nyinginezo	6.4	6.7	6.5	7.5	5.8	6.0	4.6	5.2	4.3	4.7
Pato la Taifa	**6.7**	**9.3**	**5.2**	**7.0**	**4.7**	**7.6**	**6.6**	**6.7**	**7.4**	**7.1**

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2014

1.4 Idadi ya Watu na Pato la Kila Mtu

Pato la Taifa mwaka 2013 lilikuwa shilingi milioni 53,174,678 kwa bei za mwaka husika, na idadi ya watu ilikadiriwa kuwa 44,827,757 mwaka 2013. Hivyo, Pato la wastani la kila mtu lilikuwa shilingi 1,186,200 kwa bei ya mwaka husika ikilinganishwa na shilingi 1,025,038 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025, kuwa na pato la wastani kwa kila mtu la Dola za Kimarekani 3,000 sawa na shilingi 4,837,184, juhudi kubwa zinahitajika kuhakikisha kuwa Pato la Taifa linaongezeka kwa kasi zaidi.

1.5 Mfumuko wa Bei

Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2014, mfumuko wa bei nchini umeendelea kubakia katika kiwango cha tarakimu moja licha ya kuwa umeongezeka kidogo kama inavyoonekana katika **kielelezo Na. 2**. Katika robo ya kwanza (Januari- Machi) 2014, mfumuko wa bei ulikua katika wastani wa asilimia 6 na katika kipindi cha robo ya pili (Aprili –

Juni) 2014 wastani wa mfumuko wa bei uliongezeka kidogo na kuwa asilimia 6.4. Aidha, mfumuko wa bei uliendelea kuongezeka na kufikia asilimia 6.7 mwezi Agosti 2014 na kushuka kidogo hadi asilimia 6.6 mwezi Septemba 2014. Hii ni kutokana na kupungua kwa mfumuko wa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kutoka asilimia 8.8 Agosti 2014 hadi asilimia 8.5 Septemba 2014. Mfumuko wa bei ambao haujumuishi vyakula na nishati kwa Septemba 2014 ulikuwa asilimia 3.1.

Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Jan – Sept 2014)



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2014

1.6 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Afrika Mashariki

Katika nchi za Afrika Mashariki mfumuko wa bei uliendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja katika kipindi cha Januari 2014 hadi Septemba 2014. Wastani wa mfumuko wa bei kwa nchi zote za Afrika Mashariki ulishuka kutoka asilimia 5.9 Januari 2014 hadi wastani wa asilimia 3.9 Septemba 2014. Hii ni kutokana na kuwepo kwa chakula cha kutosha na upatikanaji wa nishati katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa upande wa nchi za Rwanda na Burundi mfumuko wa bei ulikuwa chini ya asilimia 5 katika kipindi cha Januari 2014 hadi Septemba 2014 na Uganda mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 5.9 Januari 2014 hadi asilimia 1.4 Septemba 2014. Kwa nchi ya Kenya, mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 7.2 Januari 2014 hadi asilimia 8.3 Agosti 2014 na kushuka hadi asilimia 6.6 Septemba 2014.

1.7 Ujazi wa Fedha na Karadha

Katika mwaka 2014/15, sera za fedha ziliendelea kudhibitiwa ili ujazi wa fedha uwe katika malengo yaliyowekwa. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulipungua kutoka asilimia 16.9 Julai 2013 hadi asilimia 12.9 Julai 2014. Hii ilitokana na kupungua kwa ukuaji wa amana za hundi ambazo zilikua kwa asilimia 5.8 Julai 2014 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 24.7 Julai 2013. Vilevile, kupungua kwa M3 kulisababishwa na Serikali kupunguza kiwango cha kukopa katika mfumo wa mabenki kutoka Shilingi bilioni 1,192.9 Julai 2013 hadi Shilingi bilioni 441.3 Julai 2014.

Katika kipindi kilichoishia Julai 2014, ukuaji wa kiwango cha mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa sekta binafsi ilikuwa ni asilimia 21.1 ikilinganishwa na asilimia 16.1 Julai 2013. Hali hiyo ilisababishwa na Serikali kupunguza kukopa katika mfumo wa mabenki na hivyo fursa hiyo kutumika na sekta binafsi. Mikopo iliyotolewa kwa biashara na watu binafsi iliendelea kuchukua nafasi kubwa ikilinganishwa na mikopo iliyotolewa kwa ajili ya shughuli nyingine. Mchanganuo wa mikopo iliyotolewa na benki za kibiashara kwa sekta mbalimbali katika kipindi cha Julai 2014 ni kama ifuatavyo: shughuli za biashara asilimia 21.0; watu binafsi asilimia 17; uzalishaji viwanda asilimia 11.8; kilimo asilimia 10.0; shughuli za mawasiliano na uchukuzi asilimia 7.7; majengo na ujenzi asilimia 5.4; na mahoteli na migahawa asilimia 3.8.

1.8 Mwenendo wa Viwango vya Riba

Katika kipindi kilichoishia robo ya pili, Juni 2014, viwango vya riba vilivyokuwa vinatozwa katika benki za biashara kwa ujumla vilionesha kushuka. Wastani wa kiwango cha riba za amana za muda maalum kilipungua kidogo kutoka asilimia 8.72 Machi 2014 hadi asilimia 8.10 Juni 2014. Aidha, kiwango cha riba za amana kiliendelea kushuka hadi asilimia 7.99 Julai 2014. Vilevile, wastani wa kiwango cha riba za mikopo kilipungua kutoka asilimia 16.47 Machi 2014 hadi asilimia 16.38 Juni 2014. Hadi Julai 2014, wastani wa kiwango cha riba za mikopo uliendelea kushuka na kufikia asilimia 16.21. Kwa upande wa riba za amana za akiba, wastani uliendelea kuwa asilimia 3 katika kipindi cha kuanzia Januari 2014 hadi Julai 2014. Kutokana na mwenendo huo wa

viwango vya riba, tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja iliongezeka kutoka wastani wa asilimia 2.79 Juni 2013 na kufikia asilimia 3.59 Juni 2014.

1.9 Thamani ya Shilingi

Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani iliendelea kupungua katika kipindi chote kuanzia Januari 2014 hadi Agosti 2014, ambapo Dola moja ya Kimarekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 1,610 Januari 2014 na shilingi 1,666.0 Agosti 2014. Kupungua kwa thamani ya shilingi kulitokana na kuongezeka kwa mahitaji makubwa ya Dola ya Kimarekani kwa ajili ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka nje.

1.10 Sekta ya Nje

Katika mwaka unaoishia Julai 2014, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma nje ulikuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2013. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 6.4 kutoka Dola za Kimarekani milioni 8,675.6 Julai 2013 hadi Dola milioni 8,895.4 Julai 2014. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa zisizo za asilia ambazo ni bidhaa za viwandani na mapato yatokanayo na usafirishaji. Thamani ya mauzo ya bidhaa viwandani iliongezeka kwa asilimia 25.9 kutoka dola za kimarekani 1,013.1 Julai 2013 hadi Dola za Kimarekani 1,275.3 Julai 2014. Thamani ya mapato yatokanayo na shughuli za usafiri na usafirishaji yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 1,788.2 Julai 2013 hadi Dola za Kimarekani 1,998.7 Julai 2014.

Katika kipindi kinachoishia Julai 2014, thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ilifikia Dola za Kimarekani milioni 14,022.2 sawa na ongezeko la asilimia 8.8 kutoka katika kipindi kama hicho mwaka uliopita. Ongezeko la bidhaa na huduma nje lilitokana na uagizwaji mkubwa wa bidhaa za kati hususan bidhaa za mafuta, bidhaa za kukuza mitaji ikiwemo vifaa vya usafiri na mitambo.

1.11 Akiba ya Fedha za Kigeni

Katika kipindi kinachoishia Julai, 2014, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka na kufikia Dola za Kimarekani milioni 4,639.4 ikilinganishwa na Dola milioni 3,865.7 kwa kipindi kama hicho mwaka 2013. Kiasi hiki

kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.5 ikilinganishwa na miezi 4.3 mwaka 2013.

1.12 Mapato na Matumizi ya Serikali

Katika mwaka 2013/14, jumla ya mapato yote ya Serikali yakijumuisha ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 10,253, sawa na asilimia 89 ya lengo sawa na ukuaji wa asilimia 21 ikilinganishwa na mwaka 2012/13. Mapato yatokanayo na kodi yalifikia asilimia 90 ya malengo. Upungufu huo ulitokana na kutofikiwa kwa malengo katika vyanzo vyote vya kodi ukiondoa kodi ya mapato (PAYE). Malengo ya kodi hayakufikiwa kutokana na wananchi kutoitikia wito wa kutumia mashine za kieletroniki za ukusanyaji wa kodi, na kushindwa kutekelezwa kwa maboresho yaliyopendekezwa katika kuongeza wigo na mapato hususan katika tozo ya kadi ya simu.

Kwa upande wa matumizi, katika mwaka 2013/14 jumla ya matumizi yote yalikuwa shilingi bilioni 13,891.81, sawa na asilimia 83 ya makadirio ya bajeti. Kati ya hizo, shilingi bilioni 10,032.12 zilitumika katika matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na asilimia 91 ya makadirio. Matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 3,859.69 sawa na asilimia 68 ya makadirio. Matumizi katika bajeti ya maendeleo hayakuweza kufikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kutokufikiwa kwa malengo ya kukopa mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje na fedha za nje za kutekeleza miradi ya maendeleo kutotolewa kwa wakati.

1.13 Deni la Taifa

Hadi Juni 2014, deni la Taifa lilifikia shilingi bilioni 30,892.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 25,008.3 katika kipindi kinachoishia Juni 2013. Ongezeko hilo lilitokana na mikopo mipya yenye masharti nafuu na ya kibiashara na malimbikizo ya riba ya deni hususan kutoka nchi ambazo hazijatoa misamaha kwa mujibu wa makubaliano ya klabu ya Paris. Katika deni la Taifa, shilingi bilioni 22,870.3 ni deni la nje sawa na asilimia 74 ya deni ambapo deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 8,022.5 sawa na asilimia 26 ya deni. Mikopo hiyo ilielekezwa katika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo hasa miundombinu ya barabara na umeme.

1.14 Shabaha na Misingi ya Uchumi Jumla

Shabaha

Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha 2014/15-2016/17 ni kama ifuatavyo:-

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.2 mwaka 2014, asilimia 7.4 mwaka 2015 na asilimia 7.8 mwaka 2016;
ii. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja katika kipindi cha muda wa kati;
iii. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne;
iv. Kupunguza kasi ya ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) kufikia asilimia 15.5 mwaka 2014/15;
v. Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kutoka asilimia 18.4 ya Pato la Taifa mwaka 2013/14 kufikia asilimia 19.1 ya Pato la Taifa mwaka 2015/16, asilimia 19.8 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18;
vi. Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango; na
vii. Kuongeza mikopo kwa sekta binafsi kufikia asilimia 18.8 ya Pato la Taifa Juni 2015.

Misingi

Misingi ya Mpango kwa kipindi cha 2015/16 ni kama ifuatavyo:

i. Kuendelea kudumisha amani na umoja nchini na nje ya nchi
ii. Kuendelea kuimarisha Utawala bora na wa kisheria nchini;
iii. Kuendelea kuimarisha utengamavu wa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii ikiwemo ukuaji wa Pato la Taifa, ukusanyaji wa Mapato, na mfumuko wa bei;
iv. Kuwepo kwa nishati ya umeme ya uhakika;
v. Kuendelea kusimamia deni la Taifa;
vi. Kuimarisha utekelezaji wa Sera za Fedha na Bajeti;
vii. Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji;
viii. Kuendelea kuimarika kwa uchumi wa Dunia;
ix. Kuwepo kwa hali ya hewa nzuri; na
x. Utengamavu wa bei ya mafuta katika soko la dunia.

SURA YA PILI

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa

Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Juni 2014, mafanikio mbalimbali yamepatikana katika sekta zinazotekeleza miradi ya Matokeo Makubwa Sasa: kilimo, uchukuzi, nishati, elimu, maji, na fedha.

Katika **sekta ya kilimo** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:- maafisa ugani 95 kati ya lengo la maafisa 480 na wakulima 495 kati ya lengo la wakulima 195 wamepatiwa mafunzo ya kuendesha skimu za umwagiliaji; Mashamba matatu (Bagamoyo - hekta 22,000; Mkulazi - hekta 63,000; na Lukulilo hekta 5,526) yamepata hati miliki na mafunzo kuhusu biashara, kilimo bora na kuunda vyama vya wakulima yamefanyika katika miradi ya Bagamoyo, Lukulilo na Ngalimila; wakulima 1934 wamepatiwa hati za kimila kwenye mashamba ya Ngalimila na Lukulilo; na Maghala 52 yanaendelea kufanyiwa tathmini kwa ajili ya ukarabati.

Katika **sekta ya elimu** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:- wakuu wa shule za Sekondari 3,001 kati ya 3,510 kupatiwa mafunzo ya kuimarisha utendaji wa kazi zao; kufanyika kwa upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa wanafunzi wa darasa la pili; kukamilika kwa zoezi la upimaji wa shule "school ranking" ya matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na mtihani wa kidato cha nne mwaka 2012 na kuwekwa kwenye tovuti ya Baraza la Mitihani la Taifa (www.necta.go.tz) na tovuti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (www.moe.go.tz).

Katika **sekta ya nishati**, Jumla ya wateja wapya 250,340 wameunganishiwa umeme kati ya lengo la wateja 193,750 kwa kipindi cha Julai 2013 hadi Septemba 2014. TANESCO imepunguza upotevu wa umeme kutoka asilimia 21 (2012) hadi asilimia 19 (2014) baada ya kufanya yafuatayo: kufunga mita za kisasa kwa watumiaji wakubwa wa umeme zinazoendeshwa kwa mfumo wa mtandao *(Automatic Meter Reading);* Matumizi ya mita za LUKU kwa wateja wenye matumizi ya kawaida; na ukarabati wa njia za umeme na vituo vya kupozea umeme

vikiwemo vya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Gongo la Mboto, Vingunguti, Kurasini, City Centre na Mbagala.

Katika sekta ya **Uchukuzi,** mafanikio yaliyopatikana hadi mwezi Juni, 2014 ni pamoja na:- Mamlaka ya Bandari Tanzania kuvuka malengo ya kuhudumia zaidi ya tani milioni 13 Machi, 2014 ikilinganishwa na tani milioni 12 mwaka 2012. Kwa upande wa reli mafanikio yaliyopatikana ni kukamilika kwa utandikaji wa reli nzito ya ratili 80 kwa yadi kwa km 89 kutoka Kitaraka hadi Malongwe; kukamilika kwa ujenzi wa madaraja matatu ambayo madaraja mawili yako kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe na moja katikati ya stesheni za Bahi na Kintinku; kujenga upya vichwa 8 vya treni ambapo saba vimekamilika; kufanya malipo ya mwisho ya ununuzi wa vichwa vipya 13; na kukamilisha malipo ya mabehewa ya mizigo 274.

Katika **sekta ya maji,** hadi Septemba 2014, jumla ya miradi ya maji iliyojengwa na kukamilika ni 489. Idadi hii inatokana na ujenzi wa miradi 290 ya vijiji 10 katika kila Halmashauri na miradi mingine ya vijiji 199 ya upanuzi na ukarabati iliyotekelezwa chini ya programu hiyo. Miradi hiyo imevipatia maji vijiji 554 na kunufaisha watu 4,975,344; na kuongezeka kwa ufanisi katika masuala ya ununuzi wa huduma katika mikataba kutoka siku 265 hadi siku 90.

Kwa upande wa utafutaji wa **rasilimali-fedha,** Mamlaka ya Mapato Tanzania - TRA sasa inatumia kanzidata bora inayohifadhi taarifa inayoweza kuthaminisha bidhaa na hivyo kutoa makadirio bora zaidi ya viwango vya kodi; na tozo kwa ajili ya uwekezaji katika elimu umeanza Julai 2013 ikiwa asilimia 2.5 ya mapato ghafi ya kampuni za simu.

2.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati

2.2.1 Miundombinu

A. Reli

a. Kubadilisha km 197 za njia ya reli kwa kuweka reli ya kiwango cha ratili 80 kwa yadi

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kufanyika ni kukamilisha km 47

kati ya km 89 katika eneo la Kitaraka na Malongwe na kukarabati mtambo wa kuzalisha kokoto uliopo Tura mkoani Tabora. Hadi Juni 2014, mafanikio yalioyopatikana ni kukamilika kwa kazi ya kutandika reli kwa km 47 na hivyo kukamilisha km 89 za mradi, ambapo mkandarasi anaendelea na kazi za kuimarisha tuta, kuweka na kushindilia kokoto, kutengeneza mifereji na kuweka alama na mipaka ya njia ya reli; kukamilika kwa kazi ya ukarabati wa mtambo; na kukamilika kwa matengenezo ya eneo la reli kati ya Kilosa na Gulwe lililoathiriwa vibaya na mafuriko.

b. Ukarabati wa Reli (Kaliua-Mpanda)

Katika mwaka 2013/14, kazi iliyopangwa kufanyika ni kuendelea na matengenezo ya njia kati ya Kaliua na Mpanda ili huduma za reli ziweze kutolewa kwa usalama katika maeneo hayo. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014 ni kukamilika kutandikwa kwa njia ya reli yenye uzito wa ratili 56.12 kwa yadi katika maeneo yaliyopo stesheni za Lumbe kuelekea mto Ugalla na maeneo ya stesheni za mto Ugalla kuelekea Katumba; na kukamilika kwa ukarabati wa tuta la reli linalokatiza mto Ugalla na daraja lililoko km 112 kutoka Mpanda.

c. Ukarabati na Ununuzi wa Vichwa vya Treni, Mabehewa na Vifaa mbalimbali

Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2013/14 ni: kukamilisha ununuzi wa vichwa vya treni 13, mabehewa 22 ya abiria, mabehewa 274 ya mizigo, mabehewa 34 ya breki, mashine ya nyakua, toroli 30 na vifaa mbalimbali; na kujenga upya vichwa 8 vya treni, kukarabati mabehewa 125 ya mizigo, na kukarabati majengo ya karakana, stesheni pamoja na matengenezo ya njia ya reli. Mafanikio yaliyofikiwa hadi Septemba 2014 ni: kukamilika kwa kazi ya kutengeneza upya vichwa 8 vya treni ambavyo vimeanza kutumika; kukamilika kwa malipo ya ununuzi ya vichwa vipya 13; kukamilika kwa malipo ya ununuzi wa mabehewa mapya ya mizigo 274; kukamilika kwa malipo ya ununuzi wa mabehewa mapya 34 ya breki; kukamilika kwa malipo kwa Ununuzi wa Mabehewa 25 mapya ya kubebea kokoto ambayo hivi sasa yapo katika majaribio; kufanyika ukarabati wa mabehewa 82 kati ya 125 ya mabehewa ya mizigo; kukamilika kwa malipo ya ununuzi wa Mabehewa 22 mapya ya abiria; kukamilika kwa malipo kwa nunuzi wa mtambo mpya wa kunyanyulia

mabehewa na kuendelea na kazi ya matengenezo ya njia ya reli.

d. Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli

Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2013/14 ni kukamilisha ujenzi wa madaraja matatu yaliyoko km 293, km 303, na km 517 kutoka Dar es Salaam na kufanya usanifu wa madaraja yaliyo chini ya tani 15 kwa ekseli kufikia tani 25 kwa ekseli. Hadi Juni 2014, utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

i. Ujenzi wa daraja lililopo km 293 na km 303 kutoka Dar es Salaam umekamilika kwa kiwango cha kuweza kupitika na kazi inayoendelea ni ya kujenga mwelekeo wa mkondo wa maji;
ii. Ujenzi wa daraja lililopo km 517 kutoka Dar es Salaam kati ya stesheni za Bahi na Kintinku umekamilika; na
iii. Kufikia hatua za majadiliano ya kumpata mshauri elekezi wa kuchambua uwezo wa madaraja yote kwa sasa na kufanya usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa madaraja ili yaweze kupitisha tani 25.

e. Mradi wa Reli ya Kati ya Isaka – Mwanza

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kufanya usanifu wa kina wa njia ya reli kati ya Isaka – Mwanza ili iendane na kiwango cha njia ya reli kati ya Dar es Salaam - Isaka. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014, ni kufanya usanifu wa kina inayofanywa na kampuni ya COWI-Denmark.

f. Mradi wa Reli Mtwara – Mbamba Bay na Mchuchuma - Liganga

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kufanya upembuzi yakinifu wa njia ya reli kati ya Mtwara – Mbamba Bay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa kiwango cha standard gauge (mm 1,435). Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni kupatikana kwa Mtaalam mwelekezi wa kufanya kazi hii ambaye ni Kampuni ya *Dong Myeong* ya Korea Kusini.

g. Reli ya Tanga (Mwambani) – Arusha – Musoma

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kufanyika ni: kulipa fidia ya wakazi wa Mwambani; usanifu wa kina wa njia ya reli ya Tanga - Arusha; na upembuzi yakinifu wa njia ya reli ya Arusha - Musoma. Kazi zilizofanyika hadi Juni 2014 ni: kulipa fidia wakazi wapato 607 kati ya 619

ambao wamelipwa jumla ya shilingi bilioni 4.7; kufanya usanifu wa kina wa reli ya kutoka Tanga – Arusha inayofanywa na kampuni ya COWI; na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli mpya kwa kiwango cha "standard gauge" kutoka Arusha hadi Musoma inayofanywa na kampuni ya H.P. Gauff kutoka Ujerumani.

h. Ujenzi na Uboreshaji wa Reli (DSM-Isaka-Kigali)

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kufanyika ni kukamilisha upembuzi wa kina wa njia ya reli kati ya Dar es Salaam – Isaka – Kigali/Keza - Msongati. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa kazi ya upembuzi wa kina iliyotekelezwa na Mshauri mwelekezi kampuni ya CANARAIL ya Canada. Hatua inayofuata ni kumpata "Transaction Advisor" atakeyeshauri namna ya kupata wawekezaji kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi "PPP" unaendelea.

i. Usafiri wa Treni Dar es Salaam

Katika mwaka 2013/14, fedha zilitengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa njia mpya ya reli jijini Dar es Salaam. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni kuanza taratibu za kumpata mtaalam mwelekezi kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu.

B. Barabara

a. Barabara Kuu

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kujenga kilometa 495 kwa kiwango cha lami na kukarabati kilomita 190 za barabara kuu kwa kiwango cha lami. Kazi zilizofanyika hadi Juni 2014, ni kukamilisha ujenzi wa kilometa 699.15 za barabara kuu kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 141 ya lengo la kilometa 495 kwa mwaka 2013/14 na kukamilisha ukarabati wa kilometa 233 za barabara kuu kwa kiwango cha lami sawa na asilimia 123 ya lengo la kilomita 190.

b. Barabara Zenye Kufungua Fursa Kiuchumi

Katika mwaka 2013/14, miongoni mwa barabara zilizokusudiwa kujengwa na kukarabatiwa zipo katika maeneo maalum ya kufungulia ukuaji wa uchumi ambazo ni:-

i. **Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha / Songea (km 396):** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga

kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii. Hadi Juni 2014, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri zimekamilika na rasimu ya mkataba imeandaliwa na kuwasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kupata kibali.

ii. **Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 829)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na ujenzi wa barabara hii kiwango cha lami. Lengo ni kujenga barabara hii katika sehemu nne za utekelezaji ambazo ni: Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36.9) na Mpanda - Uvinza - Nyakanazi (km 582.4). Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika katika barabara ya Sumbawanga – Kanazi ni kusafisha barabara km 45, kujenga tuta la barabara km 34.8, kujenga tabaka la chini la msingi km 27.5, kujenga tabaka la juu la msingi km 25 na tabaka la lami km 25. Utekekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 47. Kazi zilizofanyika kwa barabara ya Kanazi – Kibaoni ni kusafisha barabara km 76.6, kujenga tuta la barabara km 25, kujenga tabaka la chini la msingi km 2, kujenga tabaka la juu la msingi km 0.5. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 35. Kwa upande wa barabara ya Sitalike – Mpanda kazi zilizofanyika ni kujenga tuta la barabara km 12 na kujenga tabaka la kwanza la msingi km 8. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 35. Aidha, kwa barabara ya Mpanda – Uvinza (km 195.4), usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na ujenzi utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa sehemu ya Mpanda – Mishamo (km 100).

iii. **Barabara ya Mbeya – Makongorosi – Rungwa – Itigi - Mkiwa (km 528)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na ujenzi wa barabara hii kiwango cha lami katika sehemu nne za utekelezaji ambazo ni: Mbeya - Lwanjilo (km 36), Lwanjilo - Chunya (km 36), kipande cha Chunya – Makongolo (km 43), na kukarabati barabara ya Makongolosi – Rungwa - Itigi - Mkiwa (km 413) kwa kiwango cha changarawe. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika katika barabara ya Mbeya – Lwanjilo ni kujenga tuta la barabara km 22.8 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 21; kwa upande wa barabara ya Lwanjilo – Chunya kazi zilizofanyika ni kujenga tuta la barabara km 34.31, tabaka la msingi km 25.75, na

tabaka la juu km 20.2. Utekelezaji umefikia asilimia 75. Aidha, usanifu wa barabara za Chunya – Makongorosi na Makongorosi – Mkiwa umekamilika.

iv. **Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 264.35)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na kazi ya ujenzi kiwango cha lami kwenye barabara hii katika sehemu tatu za utekelezaji ambazo ni: Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Chaya - Nyahua (km 90), na Nyahua – Tabora (km 85). Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni kujenga tuta la barabara km 84, tabaka la chini la msingi km 40, tabaka la juu la msingi km 38.35 na tabaka la lami km 37.9 katika barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 49. Kwa upande wa barabara ya Tabora – Nyahua, kazi zilizotekelezwa ni kujenga tuta la barabara km 44.4, tabaka la msingi km 35.5, tabaka la juu km 35.3 na tabaka la lami km 31.5. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 60. Kwa upande wa barabara ya Chaya - Nyahua, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea. Aidha, taarifa ya uchambuzi wa mapendekezo ya Kampuni zilizoomba kufanya kazi hii imewasilishwa *Kuwait Fund* kwa ajili ya kutoa kibali cha kuendelea na hatua ya kutangaza zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri.

v. **Barabara ya Tunduma – Sumbawanga (km 223.2)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na kazi ya ujenzi kiwango cha lami katika sehemu tatu za utekelezaji ambazo ni:- Tunduma – Ikana (km 63.7), Ikana – Laela (km 64.2), na Laela – Sumbawanga (km 93.3). Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni kukamilisha barabara za Tunduma – Ikana na Ikana – Laela. Kwa barabara ya Laela – Sumbawanga, kazi zilizofanyika ni kujenga tuta la barabara km 65.6, kujenga tabaka la chini la msingi km 62.7, kujenga tabaka la kwanza la lami km 57.8, na tabaka la pili la lami km 47.18. Kwa ujumla utekelezaji umefikia asilimia 70.5.

vi. **Barabara ya Dodoma – Babati (km 251.4)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na kazi ya ujenzi kiwango cha lami kwenye barabara hii katika sehemu nne za utekelezaji ambazo ni:- Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35), Mela – Bonga (km 88.8) na Bonga – Babati (km 19.6):

Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni kukamilika kwa ujenzi kwa barabara ya Bonga – Babati. Kwa upande wa barabara ya Dodoma – Mayamaya, kazi zilizofanyika ni kujenga tuta la barabara km 37.1, kujenga tabaka la kwanza km 35, kujenga tabaka la juu km 34 na kujenga tabaka la lami km 34.13. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 74. Aidha, katika barabara za Mayamaya – Mela na Mela – Bonga, Mikataba ya ujenzi ilisainiwa tarehe 2 Desemba, 2013 na wakandarasi wanaendelea na maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi.

vii. **Barabara ya Iringa – Dodoma (km 259.8)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na kazi ya ujenzi kiwango cha lami kwenye barabara hii katika sehemu tatu za utekelezaji ambazo ni:- Iringa – Migori km 95.1, Migori – Fufu km 93.8, na Fufu – Dodoma km 70.9. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika katika barabara ya Iringa – Migori ni kusafisha eneo la ujenzi km 86, kujenga tuta la barabara km 85.9, kujenga tabaka la kwanza la msingi km 83.1, kujenga tabaka la juu la msingi km 67.3, na tabaka la lami km 69.15. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 75. Kwa upande wa barabara ya Migori Fufu, kazi zilizotekelezwa ni kusafisha eneo la ujenzi km 93.8, kujenga tuta la barabara km 91.7, kujenga tabaka la kwanza la msingi km 72.2, tabaka la juu km 69.2 na tabaka la lami km 68.2. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 72. Aidha, kwa barabara ya Fufu – Dodoma, kazi zilizofanyika ni kusafisha eneo la ujenzi km 70.9, kujenga tuta la barabara km 70.9, kujenga tabaka la kwanza la msingi km 70.9, tabaka la juu la msingi km 70.9 na tabaka la lami km 68. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 90.

viii. **Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ililenga kukamilisha ujenzi wa barabara hii. Hadi Juni 2014, kazi zilizotekelezwa ni kujenga tuta la barabara km 53, kujenga tabaka la kwanza la msingi km 49, tabaka la juu km 46, na tabaka la lami km 42. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 93.

ix. **Barabara ya Mkiu – Itoni – Ludewa – Manda na michepuko ya Mchuchuma na Liganga (km 211):** Lengo kuu ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ili kufungua fursa za kiuchumiu

zilizopo katika kanda ya juu kusini kwenye maeneo yanayopatikana madini ya chuma eneo la Liganga na makaa ya mawe eneo la Mchuchuma. Ujenzi wa barabara hii utahusisha ujenzi wa michepuko ya barabara za Mkiu - Mndindi - Liganga - Madaba (km 46) na Mkomang'ombe – Mchuchuma (km 7). Hatua iliyofikiwa Hadi Juni 2014, Kazi za upembuzi yakinifu zimeanza na mhandisi mshauri amewasilisha ripoti ya awali.

c. Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani

Barabara zilizokusudiwa kujengwa na kukarabatiwa kwa kiwango cha lami ni zile zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Barabara hizo ni:-

i. **Barabara ya Arusha – Namanga (km 105):** Barabara hii imekamilika kwa kiwango cha lami. Hata hivyo, kazi za nyongeza za ujenzi wa kituo cha pamoja cha Forodha (*One Stop Border Post - OSBP*) zilizoanza Desemba, 2011 zinaendelea kutekelezwa. Hadi Juni 2014, kazi ya ujenzi wa kituo cha pamoja cha Forodha umefikia asilimia 96.67.

ii. **Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 165.5) na mchepuko wa Usagara – Kisesa (km 16) na Bulamba – Kisorya (km 51):** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na kazi ya ujenzi kiwango cha lami kwenye Barabara hii katika sehemu tatu za utekelezaji ambazo ni:- Mwanza/Mara Boarder – Musoma km 85.5, Kisesa – Usagara km 16, na Nansio – Kisesa – Bunda (Kisorya – Bunda) km 51. Hadi Juni, 2014, kazi zilizofanyika katika barabara ya Mara Boarder – Musoma ni kujenga tuta la barabara km 83.5, kujenga tabaka la kwanza la msingi km 81.3, kujenga tabala la juu la msingi km 80 na kujenga tabaka la lami km 76.2. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 89. Kwa upande wa barabara ya Kisesa – Usagara kazi iliyofanyika ni kukamilisha km 10.18 za tuta la barabara. Utekelezaji umefikia asilimia 8. Aidha, kwa upande wa barabara ya Kisorya – Bulambwa maandalizi ya kuanza ujenzi yanaendelea.

iii. **Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242):** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na kazi ya ujenzi kiwango cha lami kwenye Barabara hii katika sehemu mbili za utekelezaji ambazo ni:- Isaka – Ushirombo km 132, Ushirombo – Lusahunga

km 110. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni kukamilisha ujenzi kwa barabara ya Isaka – Ushirombo na kujenga kilomita 53.5 sawa na asilimia 49 kwa barabara ya Ushirombo – Lusahunga.

iv. **Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112):** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea na kazi ya ujenzi kiwango cha lami kwenye Barabara hii. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni kusafisha barabara km 80, kujenga tuta la barabara km 62, kujenga tabaka la msingi km 54, kujenga tabaka la juu km 36.8 na tabaka la lami km 32.8. Utekelezaji wa barabara hii umefikia asilimia 45.

v. **Barabara ya Arusha – Moshi – Holili pamoja na Arusha Bypass (km 140):** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuanza kazi ya kupanua barabara kuwa njia nne kiwango cha lami kwa sehemu ya Sakina – Tengeru (km 14.1) na barabara ya mchepuko (Arusha Bypass km 42.41). Hadi Juni 2014, utekelezaji wa mradi huu haujaanza kwa kuwa maandalizi ya manunuzi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu hayajakamilika.

vi. **Barabara ya Mbinga – Mbamba bay (km 66)**: Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kukamilisha usanifu wa kina na kumpata mkandarasi wa ujenzi. Hadi Juni 2014, usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Hatua itakayofuata ni kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

d. Barabara za Mikoa

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kujenga barabara za mikoa na kuendelea na ukarabati ili kuboresha barabara zinazounganisha mikoa hapa nchini. Katika mwaka 2013/14 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa km 867.6 kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa km 91.21 kwa kiwango cha lami. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni kukamilika ujenzi wa kilomita 59.25 za barabara kwa kiwango cha lami, na kukamilika ukarabati wa km 502.2 kiwango cha changarawe.

e. Barabara za Kupunguza Msongamano Mijini

Ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari ulianza katika mwaka 2009/10. Barabara hizo ni Kawawa Roundabout - Msimbazi Valley - Jangwani/Twiga Junction (km 2.7), Ubungo Bus Terminal - Kigogo - Kawawa Roundabout (km 6.4), Jet Corner - Vituka - Devis (km 10.3) na

ujenzi wa mfereji wa Bungoni unaoanzia barabara ya Nyerere hadi Uhuru (Bungoni). Pamoja na miradi hiyo, barabara zingine zinazoendelea kujengwa/kuboreshwa kwa lengo la kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam ni ujenzi wa barabara za mabasi yaendayo haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure) na vituo vyake, barabara ya Ubungo Maziwa – External (km 2.25) & Tabata Dampo - Kigogo (km 1.65), Mbezi (Morogoro Road) – Malamba Mawili – Kinyerezi - Banana (km 14), Tegeta Kibaoni – Wazo Hill - Goba - Mbezi Mwisho (km 20), Tangi Bovu - Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni (km 2.6), Kimara – Kilungule - External Mandela Road (km 9), Old Bagamoyo Road - Garden Road (km 9.1) na Kibamba – Kisopwa (Kibamba – Mlonganzila Section – km 4.0). Hadi Juni 2014, hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara ni kama ifuatavyo:-

i. Ubungo Bus Terminal – Mabibo – Kigogo Roundabout (km 6.4): Kazi ya ujenzi imekamilika, mradi upo katika kipindi cha uangalizi cha mwaka mmoja;
ii. Kigogo Roundabout – Bonde la Msimbazi – Twiga/Msimbazi Junction (km 2.7): kazi zilizofanyika ni kusafisha tuta km 2.7, kujenga tuta la barabara km 2.6, tabaka la msingi km 2 na tabaka la juu la lami km 2. Utekelezaji umefikia asilimia 75;
iii. Jet Corner – Vituka – Devis Corner (km 10.3): Mkandarasi amemaliza kazi na kukabidhi mradi tarehe 19 Septemba, 2013;
iv. Tabata Dampo – Kigogo (km 1.65) na Ubungo Maziwa - External (km 2.25): Kazi za ujenzi kwa sehemu ya Tabata Dampo – Kigogo (km 1.65) zinaendelea na kukamilika kwa sehemu ya Ubungo Maziwa – External (km 2.25);
v. Kuendelea na ujenzi wa mradi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Bus Rapid Transit Infrastructure) na vituo vyake upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-
    - *Package 1* – Ujenzi wa Barabara: Mradi unahusisha ujenzi wa barabara ya Morogoro yenye urefu wa km 15.8 kutoka Kimara hadi Kivukoni, Barabara ya Kawawa kutoka Magomeni hadi Morocco (km 3.4) na Barabara ya Msimbazi kutoka Fire hadi Kariakoo (km 1.7). Aidha, kuna vituo vya mabasi 27, vituo vikubwa *(depots)* vitatu na madaraja ya waenda kwa miguu matatu. Hadi Juni 2014, utekelezaji umefikia asilimia 65;
    - *Package 2* - Ujenzi wa Karakana na Kituo cha Mabasi cha

Ubungo: Mradi huu ulichelewa kuanza kutokana na kutopatikana kwa eneo la ujenzi hadi kusababisha mkataba kusitishwa. Hadi Juni 2014, Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu ameshaanza kazi;

- *Package 3* - Ujenzi wa Karakana (Depot) ya Jangwani: Hadi Juni 2014, maendeleo ya mradi yamefikia asilimia 70;
- *Package 4* - Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi (Terminal) Kivukoni: Hadi Juni 2014, utekelezaji umefikia asilimia 95;
- *Package 5* - Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi (Terminal) Kariakoo: Mradi ulipangwa kutekelezwa kwa miezi 12. Ujenzi unaendelea.
- *Package 6* – Ujenzi wa Vituo vya Mlisho *(Feeder Stations)*: Maendeleo ya kazi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo: Kituo cha Shekilango asilimia 25, kituo cha Magomeni Mapipa asilimia 30, kituo cha Kinondoni A asilimia 40, Kituo cha Mwinyijuma asilimia 25. Maendeleo ya mradi kwa ujumla ni asilimia 45; na
- *Package 7* – Mradi huu unahusisha kuhamisha miundombinu ya umeme kupisha ujenzi wa miundombinu ya barabara na vituo vya mabasi yaendayo haraka jijini Dar es Salaam. Kazi hizi zimekamilika.

vi. Mbezi (Morogoro Road) – Malambamawili – Kinyerezi - Banana (km 14): Mradi huu utatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ni kutoka Kinyerezi hadi Kifuru (km 4.0). Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 4 Aprili 2014 na kazi ya ujenzi imeanza tarehe 1 Oktoba 2014.

vii. Tegeta Kibaoni - Wazo – Goba - Mbezi Mwisho (km 20): Barabara hii ni kiunganisho cha barabara za pembezoni (DSM Outer Ring Road) ambayo utekelezaji wake umepangwa kufanyika chini ya mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Mkataba wa ujenzi wa barabara hii umesainiwa tarehe 4 Aprili 2014 na kazi ya ujenzi imeanza tarehe 1 Juni 2014.

viii. Tangi Bovu - Goba (km 9): Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 4 Aprili 2014 na kazi ya ujenzi imeanza tarehe 1 Juni 2014.

ix. Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni (km 2.6): Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 4 Aprili 2014 na kazi ya ujenzi imeanza tarehe 1 Juni 2014.

x. Kimara – Kilungule - External Mandela Road (km 9): Mradi huu

unatekelezwa kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza ni kutoka makutano ya barabara ya External na Mandela hadi Maji Chumvi (km 3.0). Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 4 Aprili 2014 na kazi ya ujenzi imeanza tarehe 1 Oktoba 2014.

xi. Kibamba – Kisopwa (km 12.0): Mradi huu utahusisha kipande cha Kibamba – Mloganzila (km 4.0). Mkataba wa ujenzi umesainiwa tarehe 4 Aprili 2014 na Mkandarasi yupo katika hatua ya kuweka tabaka la kati (base course)

f. Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway

Mradi huu utatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni pamoja na kutoa tangazo la kualika kampuni kuonesha nia *(Expression of Interest)* ya kushiriki katika ujenzi wa barabara hii kwa utaratibu wa PPP ambapo kampuni 12 zimeonyesha kuwa na uwezo wa kujenga barabara hiyo. Aidha, maandalizi ya kumpata Mtaalam Mwelekezi *(Transaction Advisor - TA)* atakayeishauri Serikali kuhusu utekelezaji wa mradi huu yanaendelea.

g. Madaraja

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea kujenga madaraja makubwa ya Kirumi kwenye barabara ya Makutano – Sirari, daraja la Nangoo kwenye barabara ya Mingoyo – Masasi – Tunduru, daraja la Sibiti kwenye barabara ya Ulemo – Gumanga – Sibiti, daraja la Maligisu (Mwanza) kwenye barabara ya Bukwimba – Kadashi - Maligisu, daraja la Kilombero kwenye barabara ya Mikumi - Ifakara – Mahenge, daraja la Kavuu kwenye barabara ya Majimoto-Inyonga, daraja la Mbutu kwenye barabara ya Igunga-Manonga, daraja la Kigamboni, daraja la Ruhekei kwenye barabara ya Mbinga-Mbamba Bay, daraja la Ruhuhu (Ruvuma) na ununuzi wa *'Mabey Compact Emergency Bridges* na *Crane Lorry'*. Hadi Septemba 2014, kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:

i. Kukamilika kwa madaraja ya Nangoo (Mtwara), Maligisu (Mwanza) na Ruhekei (Ruvuma);

ii. Ujenzi wa madaraja mengine upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Sibiti, Singida (asilimia 21); Kigamboni, Dar es Salaam (asilimia 60); Kilombero, Morogoro (asilimia 15); Mbutu, Tabora (asilimia 96); na Kavuu, Rukwa (asilimia 36);

iii. Daraja la Kirumi, Mara: Kazi ya usanifu wa kina imekamilika. Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kupitia usanifu na kusimamia kazi zinaendelea;
iv. Ununuzi wa 'Mabey Compact Emergency Bridge Parts na Crane Lorry'. Ununuzi wa 'Mabey Compact Emergency Bridge Parts' upo katika hatua za mwisho. Aidha, ununuzi wa 'Crane Lorry' umekamilika;
v. Daraja la Ruhuhu, Ruvuma: Kazi ya usanifu kwa ajili ya ujenzi wa daraja inaendelea; na
vi. Daraja la Momba, Mbeya: Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

h. Vivuko na Maegesho ya Vivuko

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kujenga na kukarabati vivuko mbalimbali ili kuimarisha usafiri na usalama majini. Hadi septemba 2014, kazi zilizofanyika ni:-

i. Ujenzi wa kivuko cha MV Malagarasi umekamilika na ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo unaendelea nchini Bangladesh. Ukarabati wa vivuko vya MV Chato, MV Kome 1, MV Geita na MV Magogogo umekamilika.
ii. Ujenzi wa maegesho ya Kahunda, Maisome na Msangamkuu umekamilika. Ujenzi unaendelea kwa kivuko cha Kilombero.
iii. Kuendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata makandarasi wa ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Kilambo (Mtwara), Ukara (Mwanza), Ilagala, Bugolora (Mwanza) na maegesho ya vivuko vya Magogoni, Jangwani Beach na Rungwe Oceanic.

C. Bandari

a. Bandari ya Dar es Salaam

Katika mwaka 2013/14, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kuboresha Bandari ya Dar es Salaam ili kuwa lango kuu la biashara kwa soko la ndani na kwa nchi jirani na kuongeza uwezo wa kuhudumia shehena kwa ufanisi. Hatua iliyofikia hadi Juni, 2014 ni: kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu wa gati nambari 1 hadi 7 na kusainiwa kwa makubaliano na Benki ya Dunia ya kuongeza kina gati nambari 1 hadi 7

na upanuzi wa njia ya kuingilia bandari ya Dar es Salaam; kutangazwa kwa zabuni ya kuendeleza mradi wa gati 13 na 14; na kutangazwa kwa zabuni kwa ajili ya kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kufanya upimaji wa udongo na miamba katika lango la kuingilia meli bandarini.

b. Bandari Kavu ya Kisarawe, Pwani

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizolengwa katika mradi huu ni kukamilisha upembuzi yakinifu awamu ya pili; kuanza usanifu wa kina na kuandaa michoro; na kufanya uthamini kwa ajili ya kulipa fidia kwa eneo la mradi lenye hekta 1,468. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni: Kupatikana kwa Mtaalam Mshauri ambaye ni Kampuni ya *Royal Haskoning* ya Uholanzi.

c. Bandari ya Mwambani - Tanga

Katika mwaka 2013/2014, kazi zilizopangwa ni kukamilisha usanifu wa kina, kuandaa michoro, pamoja na kuendelea kutafuta wawekezaji. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni kutangazwa kwa zabuni kwa wawekezaji wenye nia ya kuendeleza mradi huu kwa njia ya "Design Build Finance".

d. Bandari ya Mtwara

Katika mwaka 2013/14, Mamlaka ya Bandari Tanzania imeendelea na hatua ya pili ya usanifu wa kina, kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, kufanya tathmini ya fidia na taratibu za umiliki wa ardhi. Hatua iliyofikiwa hadi Juni, 2014 ni kutangazwa kwa zabuni kwa wawekezaji watakaoendeleza bandari hii kwa njia ya "Design Build Finance".

e. Bandari ya Kigoma

Katika mwaka 2013/14, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kuendelea na upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuboresha bandari ya Kigoma na kutwaa maeneo zaidi kwa ajili ya upanuzi wa bandari. Hadi Juni 2014 hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni kukamilika kwa kazi ya uthamini wa mali eneo la Kibirizi lenye hekta 10 kwa ajili ya upanuzi wa bandari; na kupatikana kwa Mtaalam Mshauri (M/S Royal Haskoning H.D.V Nederland, B.V) atakaefanya kazi ya Upembuzi Yakinifu. Aidha, kazi ya uthamini wa mali imekamilika kwa eneo la Katosho lenye hekta 69 kwa ajili ya kujenga bandari kavu.

f. Bandari ya Mbegani - Bagamoyo

Katika mwaka 2013/14, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilipanga kuendelea na uthamini wa mali na kulipa fidia, kufanya usanifu wa kina na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya Mbegani na kuendelea kushirikiana na wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika bandari hiyo. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014, ni kusainiwa kwa makubaliano ya kuendeleza mradi (Implementation Agreement) kati ya Serikali na Kampuni ya *China Merchants Holdings International Limited* (CMHI). Aidha, alama za mipaka ya eneo zimeainishwa, ripoti ya uthamini imekamilika na Mthamini Mkuu wa Serikali *(Chief Government Valuer)* ameihakiki na kuridhia.

D. Nishati

a. Mradi wa Bomba la kusafirisha Gesi Asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam

Ujenzi wa bomba la gesi lenye urefu wa km 542 na kipenyo cha inchi 36 kutoka Mnazi bay (Mtwara) na Songo Songo (Lindi) hadi Dar es Salaam na uwekaji wa mkongo wa mawasiliano uliendelea ambapo, kilomita 441 zimekamilika. Vilevile, ujenzi wa bomba la baharini kati ya Songosongo (Lindi) hadi Somangafungu (Lindi) lenye urefu wa kilomita 25.6 umekamilika. Aidha, ujenzi wa mitambo ya kusafisha gesi ulifikia asilimia 80 katika eneo la Madimba (Mtwara) na asilimia 73 kwa upande wa Songo Songo (Lindi). Kwa jumla utekelezaji wa mradi wote wa miundombinu ya gesi umefikia asilimia 88.

Kazi nyingine zilizofanyika katika mradi huo ni ujenzi wa nyumba za kuishi wafanyakazi katika maeneo ya mitambo ya Madimba (Mtwara) na SongoSongo (Lindi). Idadi ya majengo ni nyumba 16 kwa kila mtambo na zina uwezo wa kukaa watu 86 na ambazo ujenzi wake umefikia asilimia 99. Ujenzi wa vituo vya kupokelea gesi eneo la Somanga (Lindi) umefikia asilimia 51, Kinyerezi (Dar es Salaam) umefikia asilimia 61 na Tegeta (Dar es Salaam) umefikia asilimia 47. Kazi ya kupitisha bomba chini ya Mto Rufiji iliendelea, ambapo ujenzi unafanyika kwa njia ya uchorongaji urefu wa Kilomita moja kutoka kijiji cha Nyamwage hadi kijiji cha Mtanange.

b. Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi I (MW 150)

Katika mwaka 2013/14 malengo ya mradi yalikuwa ni: kujenga majengo ya mitambo; kujenga kituo cha kupoozea umeme na miundombinu yake; ununuzi, usafirishaji na ufungaji wa mitambo pamoja na vifaa vitakavyotumika katika uzalishaji wa umeme. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilika kwa ufungaji wa mitambo miwili yenye jumla ya MW 75 na miwili imewasili nchini kutoka Texas, Marekani; ujenzi wa matanki mawili (2) ya kuhifadhia mafuta kwa matumizi ya dharura umekamilika kwa asilimia 80; na ujenzi wa majengo ya utawala umekamilika kwa asilimia 80, karakana asilimia 60 na kukamilika kwa miundombinu ya barabara.

c. Mtambo wa Kufua Umeme Kinyerezi II (MW 240)

Katika mwaka 2013/14, malengo katika mradi huu yalikuwa ni: kukamilisha nyaraka za miradi ikiwemo mikataba ya mikopo kati ya Serikali na Wafadhili. Serikali imeendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Katika kipindi cha mwaka 2013/14 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha majadiliano ya mkopo wa asilimia 85 ya gharama ya mradi kati ya Serikali na Benki za Sumitomo Mitsui Banking Corporation (SMBC) na Japan Bank of International Cooperation (JBIC) za Japan. Gharama ya mradi ni Dola za Marekani milioni 344 sawa na Shilingi bilioni 564.

d. Mradi wa Makaa ya Mawe Kiwira - Mbeya (MW 200)

Katika mwaka 2013/14, malengo ya mradi huu yalikuwa ni kulipa madeni yote na kuendelea na taratibu za kupata mwekezaji. Katika kipindi hicho, kazi zilizofanyika ni kukamilisha malipo ya madeni ambapo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii NSSF na Benki ya CRDB walilipwa madai yao yote. Kwa sasa Serikali imekwishakabidhiwa mradi huu kutoka Kampuni ya TanPower Resource Ltd. Aidha, taarifa za kitaalamu za utafiti, upembuzi yakinifu na mazingira zilizofanyika miaka ya nyuma zilipitiwa upya. Serikali imeendelea na taratibu za kuandaa nyaraka za kumpata mwekezaji wa kuendeleza mradi unaojumuisha mgodi, mitambo ya kufua umeme wa MW 200 na ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme umbali wa kilomita 100 kutoka eneo la mradi hadi Uyole (Mbeya).

e. Umeme wa Msongo kV 220 Makambako - Songea

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga: kufanya uthamini wa mali zilizoko ndani ya njia kuu ya kusafirishia umeme, na kulipa fidia; kusafisha njia kuu ya umeme (220kV) yenye umbali wa kilomita 250, kuanza maandalizi ya ujenzi wa kilomita 900 za njia za usambazaji umeme wa msongo wa kV 33 pamoja na maeneo ya kujengea vituo viwili vya kupoozea umeme wa msongo wa kV 220/33 eneo la Madaba na Songea. Katika kipindi cha mwaka 2013/14 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kusainiwa kwa mkataba Januari 2014 kati ya TANESCO na Kampuni ya Isolux ya Hispania kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na kuunganisha wateja; kukamilisha uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme kutoka Makambako – Songea na kuwasilisha maombi ya *no objection* Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida); na kukusanya taarifa za utambuzi kwa maeneo ya wateja *(GPS – Coordinates)* kwa ajili ya usanifu*.* Aidha, ulipaji fidia kwa watakaopisha mradi katika maeneo ya Mkoa wa Ruvuma umekamilika na uhakiki wa malipo kwa Mkoa wa Njombe unaendelea.

f. Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa - Shinyanga

Mradi huu unahusika na ujenzi wa kilomita 670 wa njia ya umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Iringa - Shinyanga na ujenzi wa vituo vikuu vya kupoozea umeme (kV 400/220/33) wa gridi na njia za usambazaji umeme katika miji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kupatikana kwa wakandarasi wa mradi ambapo mikataba ilisainiwa rasmi Novemba, 2013 kati ya TANESCO na Kampuni za KEC International Limited na Jyoti Structures Limited za India na kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyosalia kwenye Wilaya za Igunga, Kishapu na Shinyanga. Vilevile, kazi za upimaji (detailed survey), utayarishaji, usanifu na uidhinishaji wa michoro zinaendelea. Ununuzi na usafirishaji wa vifaa vya ujenzi wa njia za umeme umekamilika kwa asilimia 90. Kazi ya ujenzi wa misingi ya nguzo za umeme imefikia asilimia 37 kwa sehemu ya Singida-Shinyanga na asilimia 35 kwa sehemu ya Iringa – Dodoma.

g. Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 400 (North – West Grid)

Mradi huu unahusika na ujenzi wa njia ya umeme kutoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 1,148. Awamu ya kwanza ya mradi huu inahusika na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 340 kutoka Mbeya hadi Sumbawanga, na vituo vikubwa vipya vya kupoozea umeme vya Mbeya (sehemu ya Uyole) na Sumbawanga.

Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilika kwa kazi ya kupitia upya Taarifa ya Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii (ESIA) iliyofanyika Oktoba, 2013; kupatika kwa mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuboresha upembuzi yakinifu kutoka msongo wa kV 220 kwenda kV 400; na upimaji wa mkuza kwa ajili ya njia ya umeme na kuandaa tathmini ya fidia ya mali kwa awamu ya kwanza ya mradi eneo la Mbeya - Sumbawanga.

h. Miradi ya Umeme Vijijini

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuendelea kusambaza umeme vijijini kupitia TANESCO na Wakala wa Nishati Vijijini (REA). Pamoja na juhudi nyingine, Serikali ilitekeleza Awamu ya Kwanza ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini uliokuwa na miradi midogo 41 katika mikoa 16 ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga. Vile vile, Wakala wa Nishati Vijijini imesaini mikataba 35 na wakandarasi 16 wa kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara.

i. Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma - Njombe

Katika mwaka 2013/14, malengo ya mradi huu yalikuwa ni kukamilisha tathmini ya athari za mazingira na kulipa fidia kwa wananchi waishio eneo la mradi. Hadi Juni, 2014 kazi iliyofanyika ni kukamilisha utafiti juu ya athari za mazingira na kijamii, kuanza majadiliano na TANESCO juu ya uuzaji wa umeme, na kuomba leseni ya kuchimba madini. Mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kuzalisha umeme megawati 600, ambapo megawati 300 zitatumika katika mradi wa chuma Liganga, na megawati 300 zitaingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Utafiti unaonesha kuwa katika

mgodi huu kuna zaidi ya tani milioni 428.36. Mradi mzima utagharimu Dola za Marekani bilioni 1.2, sawa na Shilingi bilioni 1,920.

j. Mradi wa Makaa ya Mawe Ngaka – Ruvuma

Mradi wa makaa ya mawe Ngaka unatekelezwa na TANCOAL Energy Limited ambayo ni kampuni ya ubia kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Shirika la Maendeleo ya Taifa na kampuni ya Intra Energy ya Australia. Lengo la mradi huu ni kufua umeme wa MW 200 katika awamu ya kwanza. Umeme utaingizwa kwenye gridi ya Taifa baada ya kukamilika kwa njia ya usafirishaji umeme ya Makambako – Songea yenye msongo wa kV 220. Hadi Juni, 2014 majadiliano kati ya TANESCO na Kampuni ya TANCOAL yameendelea kufanyika kuhusu mauzo ya umeme wa MW 200 unaotarajiwa kufuliwa. Mradi huu utagharimu takriban Dola za Marekani milioni 400, sawa na Shilingi bilioni 640.

E. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

a. Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kufanyika ni: kuelimisha umma kuhusu mfumo mpya wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta; kuhamasisha taasisi, makampuni mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuchangia katika utekelezaji wa mradi huu; na kuwezesha utekelezaji katika mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014 ni: Kukamilisha mwongozo wa uwekaji majina ya mitaa na uwekaji namba za nyumba na kuanza mpango wa utekelezaji kwa mkoa wa Dar es Salaam; majina ya mitaa katika kata kumi zilizochaguliwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji katika manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni (5-Ilala, 3-Kinondoni na 2-Temeke) yameainishwa na utekelezaji umeanza Disemba 2013, ambapo utekelezaji utaendelea katika kata thelathini kwa lengo la kukamilisha kata arobaini; kubandika vibao vya anwani za makazi na Misimbo ya Posta katika ofisi arobaini (40) za Wizara na baadhi ya taasisi za Serikali zilizoko jijini Dar es Salaam; na mwongozo wa Anuani za Makazi na Misimbo ya Posta unaandaliwa.

b. Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Katika mwaka 2013/14, shughuli zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kujenga awamu ya III sehemu ya kwanza inayohusu kupanua mkongo kwa baadhi ya maeneo ambayo hayakufanifikiwa katika awamu ya I na

ya II; kujenga vituo vya kumbukumbu Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar; kujenga 'IP Network' itakayoongeza uwezo wa mkongo katika kumfikia mtumiaji wa mwisho; na kufanya tathimini ya kimazingira. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni: kufanyika kwa tathimini ya kimazingira ya awali ya Awamu ya III; na kujengwa jumla ya km 91 za mkongo katika mji wa Dar es Salaam ambazo zimeanza kutumika katika kutoa huduma.

c. Maendeleo ya TEHAMA (ICT Development)

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kufanyika ni: kuongeza vifaa kwenye vituo vya mawasiliano vya Ludewa na Isaka; kuendelea kusaidia uwekaji wa mtandao wa kompyuta kwenye vituo vitano vitakavyokidhi vigezo vilivyowekwa na kuviunganisha katika mtandao; kutoa mafunzo kwa waratibu wa vituo vya mawasiliano ili kuwaongezea uwezo wa kuviendesha; kuelimisha umma juu ya umuhimu wa vituo vya mawasiliano; na kuratibu na kuwezesha uendelezaji wa mradi wa PAN-African e-network ikiwemo afya mtandao. Hatua ya utekelezaji hadi Juni 2014 ni:- kukamilika kwa mwongozo wenye kuelekeza mfumo wa uanzishaji, usimamiaji, uendeshaji na uendelezaji wa vituo vya mawasiliano nchini Februari 2014; na kuandaliwa kwa rasimu ya andiko jipya la mradi wa maendeleo ya TEHAMA.

d. Maeneo Maalum ya TEHAMA

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuanza ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo *high connectivity facility*, barabara, maji na umeme katika kijiji hicho cha kisasa cha mawasiliano ambacho kitachangia kuleta makampuni makubwa ya kimataifa kuwekeza na hatimaye kuweza kukuza uchumi unaoongozwa na maarifa. Hatua ya utekelezaji hadi Juni 2014 ni pamoja na kupatikana kwa eneo lenye ekari 438 kwa ajili ya kuanzisha Kijiji Mahiri cha TEHAMA (Smart ICT Village) Bagamoyo, Pwani.

F. Maji Safi na Maji-taka

a. **Mradi wa Maji wa Ruvu Chini – Pwani:** Katika mwaka 2013/14, Serikali ililenga kukamilisha upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji katika eneo la mradi; na kukamilisha ujenzi wa bomba kuu kutoka Ruvu chini hadi kwenye matanki yaliyopo maeneo ya Chuo Kikuu cha Ardhi. Mradi huu utakapokamilika

utaongeza uwezo wa sasa wa uzalishaji wa mita za ujazo 182,000 hadi mita za ujazo 272,000 kwa siku ili kukidhi mahitaji ya maji hadi mwaka 2032. Hadi Septemba, 2014 kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji; na utandazaji wa mabomba kutoka Bagamoyo hadi Dar es Salaam umekamilika kwa kilomita 48 kati ya kilomita 55.93 za mradi wote sawa na asilimia 85.

b. **Mradi wa Maji Ruvu Juu – Pwani:** Katika mwaka 2013/14, mradi ulilenga kupata msimamizi na mkandarasi wa ujenzi kwa ajili ya upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji na ujenzi wa njia ya kusafirisha maji kutoka Ruvu Juu hadi Kimara, Dar es Salaam. Mradi huu utaongeza uwezo wa sasa wa lita za ujazo 82,000 hadi lita za ujazo 196,000 kwa siku ili kukabiliana na ukuaji kasi wa miji ya Mlandizi na Kibaha pamoja na jiji la Dar es Salaam. Hadi Septemba 2014, utekelezaji kwa upande wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu hatua iliyofikiwa ni kusainiwa mkataba na Kampuni ya VA-TECH WABAG kwa ajili ya kufanya kazi za survey na utafiti wa udongo. Aidha, mkataba kwa ajili ya ujenzi wa bomba umesainiwa baina ya Serikali na kampuni ya Megha Engineering and Infrastructural Ltd Januari, 2014 na amekamilisha utafiti wa udongo na uchunguzi wa awali wa matanki ya Kibamba na Kimara.

c. **Ujenzi wa Bwawa la Kidunda – Morogoro:** Katika mwaka 2013/14, kwa upande wa ujenzi wa bwawa la Kidunda, kazi zilizopangwa kufanyika ni kulipa fidia na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 76 kutoka Ngerengere hadi bwawa la Kidunda. Hadi Septemba 2014, utekelezaji ni kukamilika kwa taarifa ya athari za kimazingira na kijamii zitakazotokana na ujenzi wa barabara kuelekea eneo la mradi; Gharama ya fidia kwa ajili ya watakaohamishwa kupisha ujenzi wa bwawa ni Shilingi bilioni 3.6 na ujenzi wa barabara ni Shilingi bilioni 3.8 ambapo Serikali imetoa Shilingi bilioni 7 za fidia hiyo. Aidha, fidia imelipwa kuanzia Julai, 2014 baada ya wananchi kukamilisha taratibu ikiwa ni pamoja na kufungua akaunti Benki. Kamati imeundwa kwa ajili ya kushughulikia malalamiko ya malipo ili kubaini usahihi wake kwa nia ya kuchukua hatua stahiki. Vilevile, DAWASA imeingia

makubaliano na Ofisi ya Mkurugenzi wa halmashauri ya Morogoro ili kuandaa viwanja 1000 kwa ajili ya kuwahamishia wananchi watakaopisha mradi pamoja na na eneo la barabara kwenda katika makazi mapya yanayoandaliwa.

d. **Mradi wa Visima Virefu vya Kimbiji, Dar es Salaam na Mpera, Pwani:** Katika mwaka 2013/14 kazi zilizopangwa katika mradi wa visima virefu vya Kimbiji, Kigamboni (Dar es Salam) na Mpera, Kisarawe (Pwani) ni uchimbaji wa visima 20 vya uzalishaji na visima vinane (8) vya kubaini mwenendo wa rasilimali za maji chini ya ardhi. Visima hivi vinatarajia kuongeza upatikanaji maji katika jiji la Dar es Salaam kwa kuzalisha mita za ujazo 390,000. Hadi Juni 2014, mkandarasi ameanza kazi ya uchimbaji wa visima virefu vinane (8) vya uchunguzi wa mwenendo wa maji chini ya ardhi na amechimba kisima kipya ili kufidia kisima cha eneo la Mwasomba kilichoharibika. Kazi ya majaribio ya wingi wa maji katika kisima hicho pamoja na kupima ubora wa maji imekamilika. Vilevile, mkandarasi ameanza kuchimba kisima cha pili eneo la Mkuranga na hadi sasa amechimba mita 200 kati ya mita 600. Aidha, ulipaji wa fidia kwenye eneo la mita 60 kuzunguka kila kisima katika maeneo ya Kimbiji na Mpera umekamilika.

e. **Mradi wa Maji Same - Mwanga - Korogwe:** Katika mwaka 2013/14, mradi huu ulilenga kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa mtambo wa kusukuma maji, ujenzi wa miundombinu katika chanzo cha maji ya bwawa la Nyumba ya Mungu, mtambo wa kusafisha maji, ujenzi wa njia ya umeme, ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji na ujenzi wa tanki kuu la kuhifadhi maji. Hadi kufikia Septemba 2014, usanifu wa mradi umekamilika na mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji amepatikana. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mkandarasi atakapokamilisha ukusanyaji wa vitendea kazi Januari, 2015.

f. **Miradi ya Maji Vijijini:** Katika mwaka 2013/14, mradi wa vijiji kumi (10) katika kila Halmashauri umelenga kujenga miundombinu ya miradi ya maji 1,473 katika vijiji 1,555 na kujenga vituo 32,274 vya kuchotea maji ili kuwanufaisha jumla ya wananchi 8,068,500.

Kutokana na msukumo wa programu ya Matokeo Makubwa Sasa, jumla ya miradi ya maji iliyojengwa na kukamilika hadi Septemba 2014 ni 489. Idadi hii inatokana na ujenzi wa miradi 290 ya vijiji 10 katika kila Halmashauri na miradi mingine ya vijiji 199 ya upanuzi na ukarabati iliyotekelezwa chini ya programu hiyo. Miradi hiyo imevipatia maji vijiji 554 na kunufaisha wananchi 4,975,344. Aidha, jumuiya za watumia maji (COWSCO's) 373 zimeundwa na kuanza kutoa huduma vijijini.

g. **Upanuzi wa Mradi wa Maji Ziwa Victoria – Shinyanga – Kahama:** Katika mwaka 2013/14, mradi ulilenga kuongeza usambazaji maji katika wilaya za Nzega, Igunga na Tabora pamoja na miji midogo ya Isaka, Kagongwa na Tinde. Hadi Septemba, 2014 usanifu wa awali kwa ajili ya miradi ya maji kwa miji ya Tabora, Igunga na Nzega umekamilika, kwa sasa Mtaalam Mshauri anaendelea kukamilisha usanifu wa mradi mzima na kutayarisha vitabu vya zabuni. Serikali imeanza mazungumzo na Serikali ya India kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Aidha, mradi wa kupeleka maji katika miji midogo ya Isaka, Kagongwa na Tinde taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri wa kusanifu mradi huu zinaendelea.

h. **Miradi ya Maji ya Kitaifa:** Katika mwaka 2013/14, Serikali ililenga kukarabati miundombinu ya maji katika miradi mikubwa saba ya Kitaifa ili kuongeza ufanisi wake. Hadi Juni 2014, Serikali imeendelea kuboresha huduma za maji kwa kununua pampu, mabomba, kukarabati miundombinu ya maji na kugharamia malipo ya umeme kwa ajili ya kuendeshea mitambo katika miradi ya Maji ya Kitaifa. Miradi hiyo ni Makonde (Mtwara), Wanging'ombe (Njombe), Kahama - Shinyanga (Shinyanga), na Maswa (Simiyu), Chalinze (Pwani), Mugango - Kiabakari (Mara), na Handeni *Trunk Main* (Tanga).

2.2.2 Kilimo

a. Kilimo cha Miwa

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa ni kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji katika kilimo cha miwa kwenye mabonde ya Wami, Ruvu,

Rufiji, Kagera, Kilombero na Malagarasi; kuandaa mpango wa kina wa matumizi bora ya ardhi katika eneo la Ukanda wa Kilimo Kusini mwa Tanzania - SAGCOT na kupima ardhi kwa ajili ya uwekezaji. Hadi Juni 2014, utekelezaji ni: kuhakikiwa kwa jumla ya hekta 254,675 ambapo mashamba matatu yenye jumla ya hekta 90,526 yalipata hati miliki katika bonde la Ruvu eneo la Bagamoyo (hekta 22,000), Mkulazi, Rufiji (hekta 63,000) na Lukulilo (hekta 5,526); kutoa hati za kimila kwa wakulima 1,934 kwenye mashamba ya Ngalimira na Lukulilo; kukamilika kwa mipango ya kina ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji vya wilaya za Kilombero na Rufiji na kutangaza mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji katika gazeti la Serikali kwa mashamba ya Tawi hekta 9,365.59 na Muhoro hekta 3,915.85. Kwa upande wa bonde la Malagarasi, mashamba mawili yamepatikana katika maeneo ya Kasulu hekta 47,000 na Kibondo hekta 25,000 ambapo Kampuni ya Kigoma Sugar imeonesha nia ya kuwekeza katika eneo la Kasulu.

b. Miradi ya Ukanda wa SAGCOT

Miradi ya Kilimo ya umwagiliaji katika Ukanda wa Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) iliyotekelezwa ni pamoja na:-

i. **Mradi wa Umwagiliaji Itete, Morogoro (Hekta 1,000):** Katika mwaka 2013/14 lengo ilikuwa ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Hadi Juni 2014, ujenzi wa ofisi ya mradi umekamilika, ujenzi wa banio umefikia asilimia 60; na ujenzi wa mfereji mkuu wa kushoto na kulia umekamilika kwa asilimia 50 na 15 kwa mtiririko huo;

ii. **Mradi wa Umwagiliaji Lupiro, Ulanga-Morogoro (Hekta 4,000):** Katika mwaka 2013/14 malengo ya mradi yalikuwa ni pamoja na kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu; usanifu na kuanza ujenzi. Hadi Juni 2014, mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa kazi ya upembuzi yakinifu. Aidha, kazi ya usanifu inayotekelezwa na wahandisi kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imekamilika kwa asilimia 80;

iii. **Mradi wa Umwagiliaji Sonjo, Kilombero - Morogoro (Hekta 1,340)** Hadi Juni 2014, kazi ya usanifu imekamilika. Kazi hii inatekelezwa na timu ya Wahandisi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; na

iv. **Kambi ya Vijana ya Kilimo Mkongo, Rufiji - Pwani:** Katika

mwaka 2013/14 Serikali ilipanga kuanzisha kambi ya mafunzo ya kilimo kwa vijana eneo la Mkongo-Rufiji. Hadi Juni, 2014 mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa ukarabati wa majengo 11 ambayo miaka ya 1970 yalikuwa yanatumika kama kituo cha utafiti wa kilimo.

c. Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni: kuanza kwa ujenzi na ukarabati wa skimu 6 za Makorora (Korogwe), Misozwe (Muheza), Ndongosi (Songea), Bugolora (Ukerewe), Namingongo (Mbozi) na Mwendamtitu (Mbarali) zenye ukubwa wa hekta 9,096; ujenzi wa mabwawa sita (6) umefikia katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Bwawa la Itagata (Manyoni) na Kasuga (Kakonko) ujenzi umekamilika; Lwanyo (Mbarali) - ujenzi wa tuta la bwawa umefikia asilimia 96; Mahiga (Kwimba) - ujenzi umefikia asilimia 95; Dongobesh (Mbulu) ujenzi umefikia asilimia 85; na Inala (Tabora Manispaa)- ujenzi umefikia asilimia 57.

d. Tafiti za Kilimo

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa katika kuimarisha tafiti za kilimo ni pamoja na kufanya tafiti mbalimbali, kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora zinazohimili ukame, na kukarabati miundombinu katika vituo vya utafiti vya KATRIN, Ukiliguru na Dakawa. Hadi Juni 2014, mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na: kufanya tafiti 4 katika masuala ya udongo na maji; kugunduliwa aina mbili za mbegu bora za mpunga zinazohimili ukame na magonjwa; na kukarabati miundombinu katika vituo vya utafiti ambapo miundombinu ya umwagiliaji katika kituo cha KATRIN - Morogoro imekamilika kwa asilimia 95, Ukiriguru kwa asilimia 85 na kituo cha Dakawa zabuni kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu imetangazwa.

e. Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Chakula

Katika mwaka 2013/14 kazi zilizopangwa ni kukamilisha ujenzi wa ghala la Songea lenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 pamoja na kuanza kwa ujenzi wa maghala mawili Songea na Mbozi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa ghala la kuhifadhia tani 5,000 za chakula - Songea; kukamilika kwa asilimia 95 ya ukarabati wa maghala 30 wilayani

Mbozi (26) na Momba (4); na kufanyiwa tathmini ya ukarabati wa maghala 52.

2.2.3 Viwanda

a. Maeneo Maalum ya Uwekezaji

i. **Eneo la Bagamoyo SEZ**: Uthamini wa eneo hili ulifanyika mwaka 2008 ambapo jumla ya fidia iliyotakiwa kulipwa ni shilingi bilioni 58.8, kwa eneo la hekta 5,742.52 (ekari 14,356.3) zilizokuwa zinamilikiwa na jumla ya watu 2,180 zilizothaminiwa. Kasi cha fidia kilicholipwa kwa mwaka 2013/14 ni shilingi bilioni 3, na kufanya jumla ya fidia iliyolipwa hadi Juni 2014 kufikia shilingi bilioni 19.9, na eneo lililolipiwa fidia ni hekta 1,964.6. Hivyo, eneo la hekta 3,777.92 halijalipiwa fidia. *Cadastral Survey* ya eneo hili inaendelea, na utafiti wa athari za mradi kimazingira (Strategic Enviromental impact assessment) umefanyika na taarifa ipo katika hatua za mwisho kukamilika.

ii. **Kulipa fidia maeneo ya EPZ/SEZ ya Tanga, Ruvuma na Kigoma:** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kulipa fidia katika maeneo ya SEZ ya Tanga, Ruvuma na Kigoma. Hadi Juni 2014, kiasi cha shilingi bilioni 3 kililipwa katika eneo la Tanga SEZ, ambapo jumla ya idadi ya watu waliolipwa ni 349 katika eneo la jumla ya hekta 700.

iii. **Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini, Dar es Salaam:** Malengo kwa mwaka 2013/14, ni ulipaji fidia yenye jumla ya shilingi bilioni 94.1. Hadi Juni 2014, kiasi cha fidia kilicholipwa ni shilingi bilioni 20 na hivyo kufanya jumla ya fidia iliyolipwa katika eneo hilo kufikia bilioni 45, kwa kaya 472. Kampuni ya YIWU Panafric International Investment ya China inatarajia kujenga kituo hicho.

b. Mradi wa Makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga

Kazi zilizopangwa kwa mwaka 2013/14, ni kukamilisha tafiti za kubaini wingi na ubora wa makaa ya mawe na chuma na kufanya maandalizi ya ujenzi wa migodi. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilika kwa uchorongaji katika eneo la Mchuchuma ambao umebaini uwepo wa mashapo ya makaa ya mawe kiasi cha tani milioni 370 katika eneo la kilometa za Mraba 30 na chuma kiasi cha tani milioni 219 katika

eneo la Kilometa za Mraba 10 katika eneo la Liganga; kukamilisha upembuzi yakinifu na michoro kwa ajili ya ujenzi wa migodi; kukamilisha taarifa ya utafiti juu ya athari za kimazingira zitakazotokana na miradi; kuanza unununzi wa mitambo, na kuanza majadiliano na TANESCO juu ya mkataba wa unununzi wa umeme (PPA) utakaozalishwa huko Mchuchuma baina ya kampuni ya ubia ya Tanzania China Mineral Resources Limited (TCIMRL), Shirika la Maendeleo la Taifa - NDC na TANESCO. Mradi unatarajiwa kuzalisha umeme megawati 600, ambapo megawati 250 zitatumika katika mradi wa chuma Liganga na megawati 350 zitaingizwa kwenye Gridi ya Taifa.

Kazi zilizoendelea hadi Oktoba 2014 ni pamoja na kuanza majadiliano na watu ambao wataathirika na mradi kumzungumzia jinsi gani ya kuwahamisha na kulipa fidia pamoja na kuanza uthaminishaji wa mali za waathirika. Aidha, Serikali kupitia TANROADS inakamilisha uboreshaji wa barabara kwenda kwenye maeneo ya miradi ili kuruhusu usafirishaji wa mitambo ya ujenzi wa miradi hii. Ujenzi wa migodi, kituo cha umeme, na kiwanda cha chuma utaanza mwanzoni mwa mwaka 2015 na uzalishaji unategemea kuanza 2018/2019.

c. Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, Pwani

Serikali kupitia NDC inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha Viuadudu vya kuulia viluwiluwi vya mbu wanaoeneza malaria kwa kutumia teknolojia ya Cuba ya Kampuni ya LABIOFAM SA. Gharama za mradi huu ni dola za Kimarekani 22,307,512 sawa na shilingi za Kitanzania 31,096,917,072 kwa kiwango cha kubadilisha fedha cha Juni 2010. Kazi zilizopangwa katika mwaka 2013/14 ni kukamilisha ujenzi wa kiwanda na kuanza uzalishaji. Hadi Juni, 2014 hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa majengo ya kiwanda; kuanza ujenzi wa barabara za kuingilia kiwandani na za ndani ya kiwanda; na kuendelea na usimikaji wa mitambo. Kiwanda hiki kiliwekewa jiwe la msingi Oktoba, 2013 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, na kinatarajiwa kuanza uzalishaji wa majaribioDisemba 2014. Kazi zinazofanyika hadi sasa ni kukamilisha ufungaji wa mitambo na mfumo wa maji pamoja maegesho ya magari, uzio, na matanki ya maji safi na machafu.

d. Mradi wa Magadi Soda- Ziwa Natron na Bonde la Engaruka

Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa ni kutafuta mtaalam mwelekezi wa kufanya utafiti yakinifu; kuchoronga mashapo 16 katika bonde la Engaruka na kufanya utafiti wa kitaalam wa athari za mradi kwa ndege aina ya Korongo (flamingo) katika Ziwa Natron. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kuendelea na tafiti za kubaini athari za mradi kuhusu mwenendo na tabia ya Korongo na kutafiti teknolojia bora za uchimbaji wa magadi soda katika mradi wa magadi soda bonde la Engaruka na Ziwa Natron. Eneo la Engaruka limebainika kuwa na magadi yenye mita za ujazo bilioni 4.68 kiasi ambacho ni kikubwa kutosheleza uchimbaji magadi soda kwa zaidi ya miaka 400. Upatikanaji wa magadi soda utasaidia kuendeleza viwanda vya kuchakata chuma, viwanda vya madawa, sabuni, nguo na rangi. Mchakato wa kumpata mtaalam mshauri kufanya usanifu wa kiwanda cha kuzalisha magadi katika Bonde la Engaruka na kumpata mbia atakayeshirikiana na NDC kuendeleza mradu huu umeanza.

2.2.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu

Katika mwaka 2013/14 malengo katika maendeleo ya rasilimali watu yalikuwa ni: kuendeleza ujuzi katika nyanja maalum na ujuzi katika mafuta, gesi, chuma, urani, na madini. Hadi Juni 2014, wataalam wapatao 374 waliendelea kugharamiwa masomo na Serikali katika nyanja maalum. Kati ya hao wanafunzi 76 wanasoma masomo katika fani ya mafuta na gesi katika ngazi za stashahada, shahada na shahada ya uzamili katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vikuu, vyuo vya Ufundi na vya Maendeleo ya Jamii.

2.2.5 Huduma za Utalii, Biashara na Fedha

a. Utalii

Katika mwaka 2013/14, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya utalii ni: kukamilisha kanuni za Tozo ya Maendeleo ya Utalii na ukusanyaji wa tozo la kitanda kwa siku (bed night levy) kupitia mamlaka ya Mapato Tanzania; kukamilika kwa Upembuzi yakinifu na Mpango wa biashara wa mradi wa ujenzi wa jengo la kitalii (Utalii House); kununua vifaa na samani kwa ajili ya Chuo cha Utalii Dar es Salaam; na kuendelea kupanga

hoteli katika madaraja mbalimbali katika mikoa ya Manyara ambapo hoteli mbili (2) zimetunukiwa kuwa za nyota nne (4) na hoteli nne (4) kuwa za nyota mbili. Aidha, idadi ya watalii waliofika nchini imeendelea kuongezeka kutoka watalii 1,077,058 mwaka 2012 hadi 1,095,884 mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 1.75. Mapato yatokanayo na sekta ya utalii yameongezeka kutoka dola za kimarekani 1,712.7 mwaka 2012 hadi kufikia dola za kimarekani 1,806.3 mwaka 2013.

b. Huduma za Fedha

Katika huduma za fedha, kwa mwaka 2013/14 malengo yalikuwa ni kuanzisha Benki ya Kilimo na kuziongezea mitaji Benki ya Rasilimali Tanzania na Benki ya Wanawake. Utekelezaji wake ni:

i. **Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB:** Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imeanzishwa mwaka 2013 kwa lengo la kuwezesha utoaji wa mikopo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi. Hadi Juni 2014, Serikali imekwishatoa shilingi bilioni 90 kwa ajili ya mtaji wa benki hiyo. Vilevile Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo ameshaanza kazi kuanzia Juni 2014, na taratibu za kukamilisha ajira zinaendelea.

ii. **Benki ya Rasilimali Tanzania – TIB:** Benki ya Uwekezaji Tanzania – TIB ilianzishwa mwaka 1970 kama Taasisi ya Fedha ya Maendeleo (Development Financial Institution-DFI). Mwaka 1995, TIB ilibadilishwa na kuwa benki ya uwekezaji ili kuongeza uwezo wa kukabiliana na changamoto ya soko. Lengo kuu ni kutoa fedha na huduma za uwekezaji za kibenki kwa wateja kwa misingi ya kibiashara. Hadi Septemba, 2014, Serikali imewezesha benki hii kufikia mtaji wa shilingi bilioni 152. Aidha, benki ilikuwa imeidhinisha mikopo yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 60 kwa ajili ya miradi miwili inayohusiana na sekta ya gesi.

iii. **Benki ya Wanawake Tanzania:** Benki ya Wanawake Tanzania ilianzishwa Julai, 2009 kwa lengo la kukuza uchumi na ustawi wa watanzania hasa wanawake. Hadi kufikia Juni, 2014, Serikali iliongeza shilingi milioni 450 ikiwa kama mtaji wa benki hiyo. Vilevile, benki hiyo imeendelea kuongeza vituo vya kutoa mikopo na kufikia 63, sambamba na hili shughuli nyingine zilizotekelezwa mpaka sasa ni utoaji wa mikopo kiasi cha shilingi bilioni 24.86 kwa

wajasiriamali 12,992 ambao 11,350 ni wanawake na 1,642 ni wanaume.

c. Biashara na Masoko

i. Kuendeleza Ujenzi wa Miundombinu ya Masoko

Katika mwaka 2013/14, Serikali kupitia Mradi wa Mfuko wa Jumuiya ya Ulaya ilikamilisha ujenzi wa masoko ya mpakani yafuatayo: Nyamugali - Wilayani Buhigwe (Kigoma), Mkenda Darajani - Songea Vijijini (Ruvuma) na Mtambaswala - Nanyumbu (Mtwara). Katika uendelezaji wa ujenzi wa masoko ya kimataifa ya Segera na Makambako Serikali imekabidhi miradi hiyo kwa Halmashauri za Wilaya husika baada ya kukamilisha maandalizi ya awali ili kukubaliana na wawekezaji katika ujenzi wa masoko hayo.

ii. Kuanzisha Soko la Mazao na Huduma za Bidhaa

Katika mwaka 2013/14 Serikali imeridhia kuanzishwa kwa Soko la Mazao na Bidhaa (Commodity Exchange Market); na kufanya tathmini ya maghala 30 yaliyopo katika wilaya ya Momba na Mbozi katika uanzishwaji wa "Collective Warehouse Based Marketing Scheme" (COWABAMA).

2.3 Miradi Mingine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi

2.3.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Katika mwaka 2013/14, malengo yalikuwa ni kuboresha elimu nchini kupitia mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa. Kupitia mfumo huo sekta ya elimu ilifanikiwa kutelekeza yafuatayo:- (i) Kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha nne kutoka asilimia 43.08 mwaka 2012 hadi asilimia 58.25 mwaka 2013 na ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba kutoka asilimia 31.0 mwaka 2012 hadi asilimia 50.3 mwaka 2013; (ii) Mafunzo ya ualimu yalitolewa kwa walimu 12,476 kati ya hao walimu 8,400 wa masomo ya hisabati na sayansi; (iii) Ukarabati wa miundombinu ya shule za Sekondari 264 katika Halmashauri 132 nchini; na (iv) Kulipwa kwa madai ya walimu wapatao 19,530 hadi Juni, 2014. Vile vile, katika mwaka 2013/14 ujenzi na ukarabati wa miundombinu ulifanyika katika vyuo vikuu vya Serikali kama ifuatavyo:-

i. **Chuo Kikuu cha Dodoma:** Katika mwaka 2013/14 malengo yalikuwa ni kukamilisha ujenzi wa madarasa na maabara ya chuo kishiriki cha Sayansi za Ardhi na chuo kishiriki cha Sayansi Asili na

Hisabati. Hatua ya iliyofikiwa ni ujenzi kukamilika kwa asilimia 65.

ii. **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Muhimbili - Dar es Salaam:** Malengo katika mwaka 2013/14 ni ujenzi wa majengo ya na miundombinu mingine ya chuo. Ujenzi wa jengo la ofisi na madarasa ya mafunzo endelevu na weledi wa kiafya ulikamilika kwa asilimia 80. Vilevile michoro ya awali ya majengo na miundombinu ya ujenzi wa kampasi mpya ya MUHAS imekamilika ambapo mazungumzo yanaendelea baina ya Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kufadhili mradi huu.

iii. **Chuo Kikuu Mzumbe:** Katika mwaka 2013/14 malengo yalikuwa ni kujenga na kukarabati madarasa, mabweni na miundombinu ya maji katika kampasi kuu ya Dar es Salaam na Mbeya. Hadi Juni, 2014 ujenzi wa jengo la ghorofa tano na uwekaji samani katika kumbi za mihadhara ulikamilika. Vile vile michoro ya ujenzi wa madarasa katika Kampasi ya Mzumbe ulikamilka.

iv. **Chuo cha Ufundi Arusha:** Katika mwaka 2013/14 malengo yalikuwa ni kukamilisha ujenzi wa jengo la uhandisi-ujenzi na umwagiliaji, kukarabati uzio wa chuo, kutafuta msanifu na msimamizi wa mradi wa uchimbaji visima na ununuzi wa samani kwa jengo la utawala. Hadi Juni 2014, ujenzi wa jengo la uhandisi–ujenzi na umwagiliaji umefikia asilimia 90 na samani kwa ajili ya jengo hilo zilinunuliwa.

v. **Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Muhimbili – Kampasi ya Mloganzila:** Kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2013/14 ni kujenga barabara ya km. 4 kutoka Kibamba CCM hadi eneo la mradi, kuweka miundombinu ya umeme katika eneo la mradi na kuanza ujenzi wa hospitali ya kufundishia. Hadi Juni 2014, mkandarasi wa kujenga hospitali ya kufundishia amepatikana na kusaini mkataba. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya maji na umeme unaendelea.

vi. **Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi:** Kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2013/14 ni ukarabati wa majengo na miundombinu katika vyuo vya maendeleo ya wananchi vya Tarime, Mwanahala, Kilwa Masoko, Mputa Masanginya, Masasi Chilala, Mto wa Mbu, Kilosa, Mahukuru na Ikwiriri. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa madarasa,

nyumba za watumishi na vyoo katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tarime; ukarabati wa nyumba za watumishi na uingizaji wa umeme kwenye nyumba za watumishi katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mwanhala; ujenzi wa mabweni, vyoo viwili, jiko, bwalo na ukarabati wa nyumba mbili za watumishi katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mputa; kukamilika kwa ukarabati wa nyumba za watumishi, madarasa,bwalo la chakula, jengo la utawala, mabweni na vyoo katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kilwa Masoko. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni: ununuzi wa matanki ya kuhifadhi maji na ukarabati wa mfumo wa maji katika vyuo sita vya maendeleo ya wananchi vya Tarime, Musoma, Msaginya, Ilula, Kisarawe na Ulembwe.

vii. **Vyuo vya Maendeleo ya Jamii**: kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa majengo ya utawala na miundombinu katika vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Mabaghai, Mlale na Misungwi. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014 ni kukamilika: ukarabati wa nyumba za watumishi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi; ukarabati wa madarasa katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeruna ukarabati wa vyoo vya wanafunzi katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba. Aidha, umeme wa gridi umeingizwa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba.

viii. **Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi - VETA:** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kujenga vyuo vya ufundi stadi katika Wilaya za Ludewa, Kilindi, Ukerewe, Namtumbo, Karagwe, Korogwe na Chunya na katika mikoa ya Geita, Njombe, Simiyu na Rukwa; ujenzi wa mabweni katika chuo cha ualimu wa ufundi stadi Morogoro; na ujenzi wa majengo ya utawala na karakana mbili za useremala katika chuo cha ufundi stadi na huduma Kihonda. Mafanikio yaliyopatikana hadi Juni 2014, ni pamoja na: taratibu za kumpata mshauri elekezi kwa Wilaya za Namtumbo na Ludewa zilifikia hatua ya tathmini na taratibu za kupata mkopo wa riba nafuu toka AfDB wa Dola za Kimarekani milioni 23 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa vyuo katika mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa ulikuwa unaendelea. Aidha, ujenzi wa majengo ya utawala na karakana mbili za useremala katika chuo cha Kihonda unaendelea.

2.3.2 Afya na Ustawi wa Jamii

i. **Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI):** Katika kuboresha utoaji wa huduma katika Taasisi ya Mifupa - MOI, Serikali ilianza utekelezaji wa awamu ya tatu wa upanuzi wa miundombinu. Awamu hii inajumuisha ujenzi wa jengo la ghorofa saba litakalokuwa na sehemu za kutolea huduma pamoja na malazi kwa wagonjwa. Hadi Juni 2014, ujenzi wa jengo umefikia asilimia 90.

ii. **Hospitali ya Taifa Muhimbili:** Kazi zilizolengwa kutekelezwa katika mwaka 2013/14 ni ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika Hospitali hii ikiwemo ununuzi wa vifaa kwa ajili ya Kituo cha Mafunzo na Tiba ya Moyo. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Kituo cha Tiba na Mafunzo ya Upasuaji Moyo.

iii. **Taasisi ya Saratani Ocean Road**
Katika mwaka 2013/2014 Serikali ilipanga kuanza ujenzi wa jengo la uchunguzi la wagonjwa, kusimika mitambo ya vifaa na ununuzi wa vifaa tiba ili kuongeza uwezo wa kutibu saratani. Hadi Juni 2014, mkandarasi amepatikana na ameandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa jengo litakalosimikwa vifaa vya uchunguzi wa Saratani.

iv. **Hospitali za Rufaa za Kikanda:** Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa hadi Juni 2014 ni: Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la tiba ya mionzi katika Hospitali ya Bugando na ununuzi wa vifaa tiba; kujenga jengo la wodi kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa ngozi, viungo na mifupa na kuboresha mfumo wa kutunza kumbukumbu katika hospitali ya Kilimanjaro Christian Medical Center (KCMC); ununuzi wa vifaa na vifaa tiba na ukarabati wa chumba cha X-rays na Wodi za wagonjwa katika hospitali ya Rufaa ya Mbeya; na maandalizi ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje yameanza ikiwemo kusawazisha na kuweka nguzo katika eneo litakapojengwa jengo la hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara.

2.3.3 Mifugo na Uvuvi

A. Mifugo

i. **Ujenzi wa Miundombinu ya Maji:** Katika mwaka 2013/14, utekelezaji wa programu Kuendeleza Sekta ya Kilimo sehemu ya Mifugo (ASDP-L) kwa upande wa Afya ya Mifugo na Binadamu

uliendelea katika Wilaya za Bahi, Chamwino, Kondoa na Kiteto. Kazi zilizopangwa katika mwaka huo ni pamoja na uchimbaji wa visima na mabwawa, ununuzi wa pampu na kuweka mabomba ya kusambaza maji. Hadi Juni 2014, mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na: kuchimbwa kwa mabwawa manne (4) katika Wilaya za Bahi (1), Kondoa (1) na Kiteto (2); Visima virefu 16 katika Wilaya za Kondoa (3), Bahi (3), Kiteto (9) na Chamwino (1) na ununuzi wa pampu na injini 6 kwa ajili ya visima hivyo.

ii. **Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Taarifa na Utambuzi wa Mifugo:** Utekelezaji wa mradi katika mwaka 2013/14 ulilenga kuimarisha mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji na kutoa elimu kwa maafisa ugani kuhusu matumizi ya mfumo huo. Hadi Juni 2014, mafanikio yaliyofikiwa ni: kukamilisha ujenzi wa mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji na kuandaa kanzidata na mafunzo ya awali kwa wataalam sita (6). Aidha, uhamasishaji wa matumizi ya mfumo wa TANLITS umefanyika katika wilaya za majaribio za Kibaha, Bagamoyo na Muheza.

iii. **Kuimarisha Taasisi za Tafiti za Mifugo:** Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika kuimarisha tafiti za mifugo ni pamoja na: kuendelea na ujenzi wa maabara ya sayansi ya nyama Mabuki, Maabara za lishe ya mifugo Mpwapwa, Tanga na 'West Kilimanjaro', kukamilisha ujenzi wa maabara ya uhawilishaji kiinitete – Mpwapwa na kuboresha vituo vipya vya kanda vya uhimilishaji vya Sao Hill na Katavi. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilika kwa ujenzi wa jengo la maabara sambamba na nyumba tatu za watumishi katika kituo cha Mabuki – Mwanza; kukamilika kwa ukarabati wa jengo la maabara ya lishe kituo cha West Kilimanjaro; ujenzi wa maabara ya maziwa TARILI-Uyole upo katika hatua za mwisho kukamilika; ukarabati wa maabara ya uhawilishaji kiinitete umekamilka; na ununuzi wa matanki ya kuhifadhia mbegu (*LN2-tanks*) kwa vituo vya Sao Hill na Katavi.

iv. **Miradi ya Kuongeza Thamani ya Mazao ya Mifugo:** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kukamilisha michoro mipya ya ujenzi wa machinjio na kuanza ujenzi. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni pamoja na

kupata Mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuanza kazi ya kupitia na kuandaa michoro ili kuendelea na ujenzi. Mshauri mwelekezi alikabidhiwa rasmi eneo la ujenzi wa machinjio ya kisasa yaliyoko Ranchi ya Ruvu tarehe 9 Aprili 2014.

B. Uvuvi

i. **Kukuza huduma za Uzalishaji wa Samaki:** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuanzisha vituo vitatu (3) vya kuzalisha vifaranga vya samaki wa maji baridi katika maeneo ya Mwamapuli - Tabora, Katonga - Kigoma na Nyamirembe – Chato (Geita) na vituo viwili vya maji ya bahari vya Mtwara na Tanga na kukarabati vituo vya Kingolwira- Morogoro, Ruhila – Songea, Mtama – Lindi, Moshi, Musoma, Mwanza, Bukoba na Mbegani-Bagamoyo. Hadi kufikia Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilika ujenzi wa bwawa la kulelea vifaranga kituo cha Mwamapuli Tabora na taratibu za manunuzi ya vifaa vya ujenzi na kuzalishia vifaranga zinaendelea. Kwa upande wa kituo cha Nyamirembe – Chato (Geita) maandalizi muhimu ikiwa ni pamoja na kusafisha eneo kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa mawili yamekamilika. Kituo cha Machui- Tanga: ujenzi wa matangi sita (6) yenye kipenyo cha mita 4.5 kwa kiwango cha zege umekamilika. Aidha, katika kituo cha Kingolwira, ujenzi wa mabwawa mawili (2) kwa kiwango cha zege na chumba cha kuzalishia vifaranga (indoor hatchery) umekamilika na ukarabati wa matanki 17 upo katika hatua za mwisho kukamilika.

ii. **Kuimarisha Taasisi zinazoshughulikia Tafiti za Uvuvi:** Katika mwaka 2013/14 malengo yalikuwa ni: kukarabati boti 2 za utafiti, ununuzi wa injini mbili za boti kwa ajili ya vituo vya Sota na Kyela na ununuzi wa vifaa vya maabara. Hadi Juni 2014, vifaa vilivyonunuliwa ni pamoja na injini mbili (2) za boti kubwa za doria, genereta, pamoja na GPS tano (5) kwa ajili ya kuimarisha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu. Aidha, taratibu za ununuzi wa boti nne (4) za doria kwa ajili ya vituo vya Mbamba Bay, Kasanga, Ikola na Igoma unaendelea.

2.3.4 Madini

i. **Ujenzi wa Ofisi za Madini za Kanda:** Serikali imeendelea na

maandalizi ya ujenzi wa ofisi za madini za kanda, ambapo lengo kwa mwaka 2013/14, lilikuwa ni kuanza ujenzi wa ofisi katika kanda za Dodoma, Katavi na Mtwara. Hadi Juni 2014, kazi zilizofanyika ni pamoja na kupatikana kwa wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Katavi na Mtwara.

ii. **Usimamizi Endelevu wa Madini na Kuimarisha Taasisi za Madini:** Lengo la mradi ni kuimarisha miundombinu ya taasisi za madini kwa kujenga maabara za kisasa za ofisi ya GST, ujenzi wa ukumbi wa mikutano wa taasisi ya utafiti wa madini, kujenga uwezo wa wachimbaji wadogo na wakati na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya wawekezaji. Hadi Juni 2014, mafanikio yaliyofikiwa ni pamoja na: kununua vifaa vya kisasa vya maabara za GST na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania; kuwezesha utoaji wa ramani za kijiolojia; kuanzishwa kwa mfumo wa kidijitali wa kuhifadhi takwimu na ramani za zamani kwa Wakala wa Jiolojia Tanzania; kuwezesha uboreshaji wa Mfumo wa Utoaji Leseni; kuimarisha mtandao wa mikoani na kuanzisha mfumo wa kisasa wa kutunza kumbukumbu za leseni za madini; na kufadhili mafunzo kwa wachimbaji wadogo.

2.3.5 Usafiri wa Anga na Majini

A. Viwanja vya Ndege

i. **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**: Katika mwaka wa fedha 2013/14, kazi zilizopangwa kufanyika ni kuanza ujenzi wa jengo la abiria pamoja na miundombinu yake (maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka) na kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014, ni:- kukamilika kwa taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa usalama na eno la maegesho ya ndege; kuendelea kwa utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kazi za ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, na usanifu wa kina kwa ajili ya upanuzi wa maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege; na kuendelea na mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya usanifu wa jengo la abiria.

ii. **Kiwanja cha Ndege cha Songwe – Mbeya:** Katika mwaka 2013/14, malengo yalikuwa ni kukamilisha jengo jipya la abiria,

jengo la hali ya hewa, uzio wa usalama, ujenzi wa tanki la maji ya akiba kwa ajili ya zimamoto na barabara ya kuzunguka kiwanja. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014, ni:- kukamilika kwa ujenzi wa jengo dogo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la zimamoto na ujenzi wa kituo cha kuchunguzia hali ya hewa. Ujenzi wa barabara ya kiunganishi kati ya wakazi wa kijiji cha Iweleje na Ikumbi umekamilika kwa asilimia 95; ujenzi wa jengo kubwa la abiria ulikuwa unaendelea na unatarajiwa kukamilika Desemba, 2014; na kukamilika kwa asilimia 50 ya ujenzi wa sehemu ya maegesho ya ndege iliyokuwa imesalia.

iii. **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza:** Kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2013/14, ni ujenzi wa jengo jipya la abiria; mnara wa kuongozea ndege; jengo la mizigo; kituo cha umeme pamoja na miundombinu yake; na urefushaji wa barabara ya kuruka na kutua ndege (mita 500). Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni pamoja na kukamilika kwa uchimbaji, ujenzi wa tabaka la mawe na ujenzi wa kalavati kubwa la kutoa maji katika eneo la kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege; kumwaga zege kutoka kwenye msingi hadi kufikia ghorofa ya kwanza katika mnara/jengo la kuongozea ndege; kukamilika kwa ujenzi wa nguzo za msingi katika jengo la mizigo; na kusafishwa kwa eneo litakalojengwa maegesho ya ndege za mizigo pamoja na viungio vyake.

iv. **Kiwanja cha Ndege cha Arusha:** Katika mwaka 2013/2014 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni maboresho ya barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani pamoja na kufanya ukarabati wa jengo la abiria. Hadi Juni, 2014 hatua iliyofikiwa ni kufungua na kufanya tathmini ya zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya marejeo ya usanifu wa miundombinu ya kiwanja pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi.

v. **Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**: Katika mwaka 2013/14 kazi zilizopangwa ni ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya kiwanja (barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kiungio); usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege, ujenzi wa jengo jipya la abiria na uzio wa usalama. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami; na ujenzi wa jengo

jipya la abiria kufikia hatua ya usimikaji wa paa na mifumo ya maji safi, maji taka na umeme; na kuendelea kwa ujenzi wa jengo la abiria na kituo cha umeme.

vi. **Jengo la III la Abiria - Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere:** Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kufanya upanuzi wa kiwanja hiki kwa kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria. Kazi zilizopangwa ni pamoja na: usanifu wa kina wa jengo na miundombinu yake, ujenzi wa uzio katika eneo la mradi, ujenzi wa ofisi za mradi, kukamilisha ujenzi wa maabara na vifaa vyake, kupima udongo, matayarisho mbalimbali ya uendeshaji, kazi za kuondoa udongo na kuweka matabaka yanayotakiwa, maandalizi ya kusimika mitambo na kuanza kwa kazi za ujenzi. Hatua iliyofikiwa hadi Juni, 2014 ni kukamilika kwa maandalizi ya ujenzi; na kuendelea kwa kazi za kuchimba na kuondoa udongo kwa ajili ya ujenzi wa msingi wa jengo la abiria.

vii. **Kiwanja cha Ndege cha Tabora:** Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kufanyika ni: ujenzi wa barabara ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege pamoja na jengo la abiria na miundombinu yake. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014, ni:- kukamilika kwa uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kukarabati barabara ya pili ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio, maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege; kuendelea kwa utayarishaji wa makabrasha ya zabuni na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege; na kuendelea kwa mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu wa kina wa jengo jipya la abiria.

viii. **Kiwanja cha ndege cha Mpanda:** Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopangwa kuafanyika ni kukamilisha deni la mkandarasi na ukamilishaji wa ujenzi wa uzio wa usalama wa kiwanja. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikiwa ni kulipwa kwa deni la mkandarasi kiasi cha shilingi bilioni 1.5 pamoja na kukamilika kwa uchambuzi wa zabuni ya ujenzi wa uzio wa usalama wa kiwanja.

ix. **Kiwanja cha ndege cha Mafia**: Katika mwaka 2013/14, kazi zilizopanga kufanyika ni:- ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio na maegesho ya ndege kwa

kiwango cha lami; ujenzi wa mfumo wa maji ya mvua na uzio wa usalama. Hadi Juni 2014, hatua iliyofikia ni; kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami; kukamilika kwa ujenzi wa mfumo wa maji; na uzio wa usalama ambapo kiwanja kilifunguliwa rasmi Oktoba 2013.

x. **Kiwanja cha ndege cha Mtwara:** Katika mwaka 2013/14 kazi iliyopangwa kufanya ni ukarabati mdogo wa njia ya kuruka na kutua ndege ili kuimarisha usalama. Hatua iliyofikiwa hadi Juni, 2014 ni kukamilika kwa ukarabati wa maeneo korofi ya barabara ya kuruka na kutua ndege.

B. Usafiri wa Majini

Katika mwaka 2013/2014 Serikali ilipanga kuendelea na ujenzi wa meli mpya 4 katika ziwa Viktoria, Tanganyika na Nyasa na ukarabati wa meli za Umoja na MV. Iringa. Hadi Juni 2014, mtaalam mwelekezi amepatikana kwa ajili ya kufanya usanifu wa ujenzi wa meli mpya 4 (Ziwa Viktoria-1, Ziwa Tanganyika-2, Ziwa Nyasa-1) na kukarabati meli 3 (MV. Viktoria, MV. Serengeti na MV. Umoja) kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark; kukamilika kwa ukarabati mdogo wa meli ya MV. Umoja na kuwasili kwa vipuri vya ukarabati wa meli ya MV. Iringa.

2.3.6 Hali ya Hewa

Katika mwaka 2013/2014, Mamlaka ya Hali ya Hewa ilipanga kukamilisha ununuzi wa rada itakayofungwa Mwanza, vifaa vya hali ya hewa na kufanya matayarisho ya ujenzi wa jengo la utabiri wa hali ya hewa. Hadi Juni, 2014 rada ya Hali ya Hewa ilikuwa imeshawasili na ufungaji unaendelea na unatarajiwa kukamilika Juni, 2014. Aidha, ufungaji wa mitambo 11 ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe katika sehemu mbalimbali nchini na upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa kituo kikuu cha utabiri umekamilika.

2.3.7 Maendeleo ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu

Katika mwaka 2013/14, Serikali ilipanga kuanzisha kituo cha Sayansi Teknolojia na Ubunifu kitakachosambaza matokeo ya sayansi na kuhawilisha fedha kwenye mashirika ya kimataifa hususan yanayohusu utafiti wa maendeleo. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2014, ni kufanyika kwa

uhawilishaji wa fedha kwenda katika mashirika ya kimataifa na kupitia upya mfumo wa Sayansi Teknolojia na Ubunifu nchini ikiwa ni pamoja na kuandaa rasimu ya programu ya mageuzi ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu nchini. Programu hii ya mageuzi katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu itawezesha mabadiliko makubwa katika miongozo ya kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubufu ikiwemo kutungwa kwa sheria ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuvutia sekta binafsi kushiriki katika kuendeleza sekta ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu.

2.3.8 Ardhi, Nyumba na Makazi

Katika mwaka 2013/14, Serikali iliendelea kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi; upimaji wa ardhi kwa ajili ya makazi na shughuli za kiuchumi ikijumuisha uanzishwaji wa Mji Mpya wa Kigamboni na kuimarisha shughuli za utafiti na maendeleo ya vifaa vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Hadi Juni 2014, rasimu ya muundo wa Wakala wa uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni na kuanzisha ofisi yake katika eneo la mradi uliandaliwa. Vilevile Mtaalamu wa Fedha (Transaction Advisor and Fund Raiser) aliteuliwa na kuanza kazi Machi 2014 ili kuongeza kasi katika kupata fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Mji Mpya wa Kigamboni.

Maeneo mengine yaliyotekelezwa ni: kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 94 kutoka wilaya mbalimbali nchini; Kanuni za Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007 iliandaliwa na kukamilika; Mwongozo wa Upangaji na Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi ulichapishwa na kusambazwa kwa wadau; na Mashine 250 za kufyatulia tofali ziliundwa. Aidha, mafunzo kwa vitendo kwa jumla ya washiriki 974 kutoka katika Wilaya mbalimbali nchini yaliendeshwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Wilaya zilizohusika na mafunzo hayo ni Sikonge (100), Biharamulo (56), Halmashauri ya Arusha (160) na Muleba (550). Pia, Mafunzo kwa vitendo yalitolewa kwa wakufunzi na wahitimu wa VETA (47), Tarime (42), Korogwe (15) na mafundi sanifu (4) kutoka manispaa ya Tabora.

2.3.9 Katiba Mpya

Katika mwaka 2013/14, Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliwasilisha rasimu ya katiba mpya ambayo ilijadiliwa na kusambazwa kwa wananchi ambao

walipata fursa ya kutoa maoni kupitia mabaraza ya Katiba. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: kuidhinishwa na Bunge kwa Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya mabadiliko ya Katiba ya mwaka 2014; na kukamilika kwa rasimu ya Katiba inayopendekezwa Oktoba 2014.

2.3.10 Vitambulisho vya Taifa

Katika mwaka 2013/14, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ililenga kutekeleza kazi zifuatazo: Utambuzi, usajili na utengenezaji wa vitambulisho vya Taifa kwa watumishi wa Serikali kwa upande wa Zanzibar na mkoa wa Dar es Salaam pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama; na kujenga mfumo wa mawasiliano kati ya ofisi za usajili za Wilaya na Makao Makuu. Hadi Juni 2014, Mamlaka imefanikiwa: kusajili wakazi 561,530 wa Unguja na Pemba, wakazi 2,165,823 wa Dar es Salaam; na wakazi 369,728 wa Pwani; kutoa vitambulisho 145,000 kwa watumishi wa umma wa Zanzibar na mkoa wa Dar es Salaam pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama; na kutolewa vitambulisho 411,000 kwa wakazi wa mkoa wa Dar es salaam. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni: Ununuzi wa vifaa vya usajili 280 (Mobile Enrollment Unit); ujenzi wa mtandao wa mawasiliano kati ya ofisi za usajili za Wilaya za Temeke, Kinondoni, Ilala, Kilombero pamoja na ofisi za Unguja na Pemba na Makao Makuu; kulipwa kwa sehemu ya deni la mkandarasi wa mradi kampuni ya IRIS ya Malaysia; na kuendelea na kazi ya kutunga sheria mpya ya utambuzi na usajili wa watu.

2.3.11 Kazi na Vijana

Serikali imeandaa programu ya miaka mitatu kwa ajili ya kukuza ajira kwa Vijana nchini iliyoanza kutekelezwa mwaka 2014/15. Programu hiyo itatoa fursa ya ajira za moja kwa moja kwa wahitimu wa elimu ya juu 300,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 540,000. Maeneo makuu ya programu ni: (i) kujenga uwezo wa vijana katika stadi za kazi na ujasiriamali; (ii) kuwapatia vijana mitaji, nyenzo na vifaa vya kufanyia kazi; na (iii) kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara. Hadi Juni 2014, kazi zilizotekelezwa ni; Kuandaa orodha ya vikundi vya vijana vya uzalishaji ambao wako tayari kuanza kutekeleza programu nchi nzima; na kuwashirikisha wadau wa maendeleo hasa ILO na UNIDO kwa ajili ya kutekeleza proramu hii.

2.3.12 Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Katika mwaka 2013/14, ujenzi wa vituo vya huduma vya pamoja mipakani (One Stop Boarder Post) uliendelea baina ya Tanzania na Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika maeneo ya Kabanga/Kobero, Horohoro/Lungalunga. Aidha, kituo cha Mutukula/ Mtukula kimekamilika na kituo cha Holili/Taveta kimeanza kutumika na kufungwa vifaa vya kisasa ili kuhakikisha kuwa ufanisi unakuwepo.

2.3.13 Sekta Binafsi

Katika mwaka 2013/14, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia sekta binafsi kushiriki katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba, 2014, Kituo cha Uwekezaji kimesajili jumla ya miradi 595, ambapo miradi 282 ni ya wawekezaji wa ndani, 142 ya wawekezaji kutoka nje na miradi ya ubia ni 171. Miradi iliyosajiliwa inatarajiwa kutoa fursa za ajira 10,054 na thamani yake ni Dola za Kimrekani milioni 11,307.

Baadhi ya miradi iliyoanza kutekelezwa katika mwaka 2013/14 ni pamoja na ujenzi kiwanda cha ngozi cha Meru Tanneries – Arusha; kiwanda cha nguo cha Dahong Shinyanga; kiwanda cha ngozi cha Xinghua Ltd – Shinyanga; kiwanda cha saruji cha Dangote – Mtwara; kilimo cha miwa Bagamoyo. Hatua zilizofikiwa hadi Juni, 2014 ni kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha ngozi Arusha chenye uwezo wa kusindika vipande 159,000 vya ngozi ya ngombe na vipande 468,000 vya ngozi ya mbuzi na kondoo kwa mwaka; kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha ngozi Shinyanga chenye uwezo wa kusindika vipande 936,000 vya ngozi ya ngombe na vipande 2,200,000 vya ngozi za mbuzi na kondoo kwa mwaka na kuajiri watu 500; na ujenzi wa kiwanda cha nguo Shinyanga kinachotarajiwa kukamilika kabla ya Disemba 2014 ambacho kitatumia pamba tani 30,000 kwa mwaka; na kuanza kwa ujenzi wa kiwanda cha saruji cha Dangote – Mtwara. Miradi mingine ya viwanda inayoendelezwa na sekta binafsi ni ujenzi wa kiwanda cha saruji Tanga kinachojengwa na kampuni ya Rhino Cement; na kiwanda cha Saruji cha MEIS - Lindi ambacho kinatarajiwa kukamilika na kuanza uzalishaji Novemba 2014. Kwa upande wa kilimo, kampuni ya Bagamoyo Eco energy imeanza hatua za awali za uwekezaji katika kilimo cha miwa eneo la Bagamoyo.

Katika juhudi za kuendeleza sekta hii, kazi zilizofanyika ni pamoja na kutoa mafunzo ya huduma za utalii huduma kwa wateja kwa maafisa 42 wa idara za usalama, forodha na uhamiaji, katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere, Kilimajiaro na Arusha, idadi ya waendesha huduma za utalii (tour operators) imeongezeka kutoka 240 Julai 2013 hadi 350 Februari 2014. Kazi nyingine zilizofanyika ni kutoa mafunzo ya mipango na ujasiriamali kwa taasisi ndogo na za kati (SMEs) 500; kununua mashine za kusindika chakula na kutoa mafunzo ya usindikaji kwa wakulima 50 na taasisi 12; kutoa mafunzo ya kilimo cha biashara kwa wakulima 250 kutoka mikoa ya Arusha na Dodoma; na mafunzo ya kilimo cha zabibu kwa wakulima 250.

SURA YA TATU

MIRADI YA KIPAUMBELE 2015/16

3.1 Utangulizi

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16 utaendelea kutekeleza programu za miradi ya kisekta kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na Malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, inapendekezwa kuwa rasilimali chache zitumike kwenye maeneo machache ya kipaumbele hususan yaliyo chini ya utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa. Katika hali hiyo miradi katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16 itaendelea kuwa katika makundi makuu mawili ambayo ni miradi ya Kitaifa ya kimkakati ikijumuisha miradi iliyo katika utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa - BRN na miradi mingine muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

3.2 Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati

3.2.1 Miundombinu

A. Usafiri na Usafirishaji

a. Reli ya Kati

i. Kuendelea kuimarisha reli ya kati hususan miradi iliyoainishwa katika programu ya Matokeo Makubwa Sasa kwa kutandika reli na mataruma mazito ya ratili 80 kwa yadi na kuondoa reli nyepesi na zilizochoka ili kuongeza uwezo wake na kuwezesha treni kusafiri kwa usalama, kasi na kubeba mizigo mizito zaidi, kutoa ajira, kukuza uchumi na biashara;

ii. Kuendelea kumtafuta mwekezaji wa kujenga upya reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa cha *standard gauge (mm 1435).* Mradi huu ukikamilika utakuza kiwango cha biashara katika nchi za Afrika Mashariki na Kati;

iii. Kuboresha miundombinu ya reli ya TAZARA kwa kukarabati karakana ya Dar es Salaam, mtambo wa kuzalisha kokoto wa Kongolo na kuboresha vituo vya abiria jijini Dar es Salaam;

iv. Kuendelea kukamilisha upembuzi wa kina na kumpata mwekezaji wa kujenga reli mpya ya Tanga – Arusha – Musoma pamoja na michepuko ya kwenda Minjingu na Engaruka. Reli hii ina mchango

mkubwa katika kukuza uchumi na biashara ya Tanzania na nchi jirani hususan Uganda na Kenya;

v. Kuendelea kukamilisha upembuzi wa kina na kumpata mwekezaji wa kujenga reli mpya ya Mtwara – Mbambabay km pamoja na michepuko ya kwenda Liganga na Mchuchuma. Reli hii itakuwa na mchango mkubwa katika kukuza uchumi na biashara ya Tanzania na nchi jirani hususan Malawi na Msumbiji. Aidha, itakuza utendaji na ufanisi wa bandari ya Mtwara.

vi. Kuendelea kuboresha usafiri wa reli jijini Dar es Salaam iikiwa ni pamoja na kufanya utafiti wa maeneo mapya ya Bunju/Kerege, Kibaha, Chamazi na Pugu.

b. Barabara

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya barabara iliyoibuliwa chini ya mfumo mpya wa Matokeo Makubwa Sasa;

ii. Kuendeleza ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami kwenye barabara zinazofungua maeneo yenye fursa za kiuchumi. Barabara hizo ni pamoja na Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 396), Barabara ya Itoni – Mkiu – Ludewa – Manda (km 211), Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Ipole – Rungwa - km 95), Barabara ya Mbeya – Makongorosi – Rungwa – Itigi-Mkiwa (km 528), Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 264), Barabara ya Tunduma – Sumbawanga (km 223.2), Barabara ya Dodoma – Babati (km 261), Barabara ya Iringa – Dodoma (km 260), Barabara ya Masasi - Songea – Mbambabay (km 1,154.7), Barabara ya Bagamoyo - Sadani – Tanga (km 178), Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60), na Barabara ya Murugarama – Rulenge – Nyakahura (km 86);

iii. Kuendelea na uboreshaji kwa kiwango cha lami kwenye barabara zinazounganisha Mikoa yote na Wilaya zote za Tanzania bara;

iv. Kukamilisha miradi ya barabara zinazopunguza msongamano katika maeneo ya mijini hususan katika Jiji la Dar es Salaam. Barabara hizo ni Ubungo Maziwa – *External* (km 2.25); Ubungo Bus Terminal – Mabibo – Kigogo *Round about* (km 6.4); *Jet Corner* – Vituka – *Davis Corner* (km 10.3); barabara ya Kigogo *Round about*-Bonde la Msimbazi –Twiga/Msimbazi *Junction* (km 2.7) na Ujenzi wa barabara ya Tabata Dampo – Kigogo (km 2.25),

Mbezi (*Morogoro Road*) – Malamba Mawili - Kinyerezi – Banana (km 14); Tegeta – Kibaoni – Wazo – Hill – Goba - Mbezi Mwisho (km 20); Tangi Bovu – Goba (km 9); Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6); Kimara – Kilungule- External Mandela Road (km 9); Kibamba- Kisopwa sehemu ya Kibamba- Mlonganzila (km 4); Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 3.2); na Ardhi – Makongo (km 4), na ujenzi wa barabara ya mabasi yaendayo haraka maeneo ya Kimara – Kivukoni, *Fire* – Kariakoo na Magomeni – Morocco (km 21.9);

v. Kuendeleza ujenzi na kuimarisha barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani. Barabara hizo ni Barabara ya Arusha – Namanga (km 105): Barabara ya Nyanguge – Musoma (km 183) na mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 17): Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242), Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza – Kobero (km 150), Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112), Barabara ya Sumbawanga – Mpanda - Uvinza – Kanyani - Kasulu - Nyakanazi na Kidahwe – Kanyani – Kasulu - Nyakanazi (Jumla km 815);
vi. Kuendeleza ujenzi wa Barabara za Juu hususan katika jiji la Dar es Salaam eneo la makutano ya Tazara pamoja na maboresho ya makutano ya barabara maeneo ya Chang'ombe, Ubungo, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, na Morocco; na
vii. Kuendeleza ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 200). Mradi huu utawezesha watumia barabara kati ya Dar es Salaam na Chalinze kusafiri kwa haraka na pia kupunguza msongamano wa magari katika barabara hiyo inayounganisha jiji la Dar es Salaam na mikoa iliyoko kanda ya kati, kaskazini na kusini mwa Tanzania. Mradi huu utatekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta binafsi na inategemewa kuongeza ufanisi katika sekta ya uzalishaji na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

c. Madaraja

i. Kukamilisha ujenzi wa daraja la Kigamboni; na
ii. Kuendelea kujenga na kukarabati madaraja ya Kirumi (Mara), Mbutu (Tabora), Maligisu (Mwanza), Sibiti (Singida), Kilombero (Morogoro), Kavuu (Rukwa), Simiyu (Mwanza), Lukuledi II

(Mtwara), Momba (Mbeya), Wami (Pwani), Ruhuhu (Songea), na Salender (Dar es Salaam).

d. Vivuko na Maegesho ya Vivuko

i. Ujenzi wa Vivuko vipya viwili na ukarabati wa vivuko vinne. Vivuko vipya ni pamoja na kivuko cha Magogoni – Kigamboni na kivuko kitakachotumika kati ya Dar es Salaam – Bagamoyo ambapo ujenzi wake unatekelezwa Bangladesh. Vivuko vitakavyofanyiwa ukarabati ni pamoja na vivuko vya MV Mwanza (Mwanza), MV Pangani II (Pangani – Tanga), MV Kiu (Kilombero) na MV Magogoni (Dar es Salaam).

ii. Ujenzi wa maegesho ya vivuko utaendelea kwa maegesho ya Kahunda - Maisome na Ilagala; kufanya upanuzi wa maegesho upande wa Kigamboni; vituo vya Magogoni, Jangwani Beach na Rungwe *Oceanic* kwa ajili ya kivuko kitakachotoa huduma kati ya Dar es Salaam na Bagamoyo; maegesho mawili (2) katika vituo vya Bukondo na Zumacheli - Geita na maegesho mawili (2) ya kivuko kitakachotoa huduma kati ya Iramba na Majita; Kilambo (Mtwara), Ukara (Mwanza), Kilombero (upande wa Ulanga - Morogoro), na Bugolora (Mwanza).

e. Bandari

i. Kuendelea kuboresha miundombinu ya bandari hususan miradi iliyoibuliwa katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa;

ii. Kuendelea kuboresha miundombinu na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kuhudumia shehena katika bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Kasanga na Kigoma;

iii. Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa bandari mpya za Mwambani (Tanga), Mbegani (Bagamoyo) na Bandari Kavu ya Kisarawe;

iv. Kuboresha mazingira yatakayowezesha sekta binafsi kuwekeza katika kujenga miuondombinu na kuboresha usafirishaji wa mizigo; na

v. Kuendelea na ukarabati na ununuzi wa vyombo vya usafiri na usafirishaji katika maziwa.

B. Nishati (Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji)

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya umeme ya kitaifa iliyoibuliwa katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa. Miradi hiyo inajumuisha: Miradi ya Uzalishaji Umeme ya Kinyerezi I (MW 150), II (MW 240), III (MW 300) na IV (MW 330); na Miradi ya Ujenzi wa Njia za usafirishaji Umeme ikiwemo mradi wa Makambako – Songea msongo wa kV 220 wenye urefu wa km 250, mradi huu pia utahusisha ujenzi wa njia za usambazaji umeme wa msongo wa kV 33 yenye umbali wa km 900; Iringa – Shinyanga, msongo wa kV 400 wenye urefu wa km 670; Upanuzi wa Gridi ya Kaskazini Magharibi *(North – West Grid Extension)*, msongo wa kV 400 kutoka Mbeya – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi yenye urefu wa km 1,148; Upanuzi wa Gridi ya Kaskazini Mashariki *(North - East Grid)*, msongo wa kV 400 kutoka Dar es Salaam – Tanga – Arusha yenye urefu wa km 682; na Singida – Arusha – Namanga, msongo wa kV 400 yenye urefu wa km 414.

ii. Miradi ya usambazaji umeme ni pamoja na mradi wa mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Shinyanga na Geita (Mradi wa *Electricity V*) yenye msongo wa kV 33 zenye urefu wa km 480, kV 0.4 km 231.

iii. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme vijijini na Makao Makuu ya Wilaya.

iv. Kuendeleza uwekezaji katika vyanzo vya nishati mbadala, jadidifu na makaa ya mawe. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa umeme wa Singida (MW 50), mradi wa kuboresha mitambo ya kuzalisha umeme Hale (MW 21) na miradi ya makaa ya mawe Kiwira (MW 200).

v. Kujenga miundombinu ya usambazaji gesi asilia katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Dar es Salaam.

C. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

i. Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupanua matumizi yake katika maeneo mbalimbali nchini na katika nchi jirani;

ii. Kuanzisha maeneo maalum ya TEHAMA;

iii. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa anuani za makazi na

misimbo ya Posta *(Physical Addressing and Post Code Systems)* katika maeneo mbalimbali nchini;

iv. Kuendeleza mradi wa Serikali mtandao;

v. Kuendeleza miundombinu na raslimali watu ili kuharakisha maendeleo ya Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi; na

vi. Kuhamasisha na kukuza tafiti za kimaendeleo.

D. Maji Safi na Majitaka

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji vijijini ambayo ipo katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa, hususan miradi ya vijiji kumi (10) katika kila Halmashauri;

ii. Upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji na kukamilisha kazi za uchimbaji wa visima vijijini;

iii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na majitaka katika Jiji la Dar es Salaam kwa kukamilisha taratibu za ujenzi katia mradi wa Kidunda, Kimbiji na Mpera na ulazaji wa mabomba katika mradi wa maji Ruvu chini na Ruvu Juu. Aidha, msukumo utawekwa katika kukamilisha miradi ya maji katika miji mingine nchini; na

iv. Kuendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na kusimamia ubora wa maji na kuimarisha bodi za maji kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji.

3.2.2 Kilimo

a. Miradi ya Matokeo Makubwa Sasa

Katika sekta ya Kilimo, miradi inayotekelezwa chini ya mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa ni pamoja na: kuanzisha mashamba makubwa 25 kwa ajili ya uwekezaji wa miwa na mpunga; usimamizi wa kitaalam wa skimu za umwagiliaji 78 na kuboresha mfumo wa soko katika skimu hizo; na kuanzisha maghala - biashara 275 ya mahindi katika maeneo mbalimbali nchini. Katika mwaka 2015/16, kazi zitakazopewa kipaumbele ni:-

i. **Uwekezaji katika kilimo cha miwa na mpunga:** Kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (*outgrowers*) wanaozunguka mashamba ya uwekezaji ya miwa na mpunga; na kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo kuhusu kilimo cha kibiashara katika mabonde ya Rufiji, Wami, Ruvu, Kagera,

Kilombero na Malagarasi yanayofaa kwa uwekezaji wa kilimo cha miwa na Mpunga;

ii. **Skimu 78 za umwagiliaji mpunga:**. Kuendelea kukamilisha ukarabati na usimamizi wa skimu 18 zenye jumla ya hekta 6,439 katika wilaya za Kyela, Sumbawanga, Mpanda, Mlele, Mbarali, Iringa, Kilombero, Mvomero, Kilosa na Morogoro Vijijini; na

iii. **Kilimo cha mahindi:** kuendelea na ujenzi wa maghala ya masoko kwa ajili ya mazao ya mahindi katika skimu za umwagiliaji zilizopo katika ukanda wa SAGCOT, hususan kukamilisha ukarabati na kuendelea na ujenzi wa maghala mapya, sambamba na kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa maghala.

b. Kambi ya Vijana ya Kilimo –Mkongo, Rufiji

Serikali itaendelea kuimarisha kambi za vijana za kilimo, ili kukuza ajira na kuwapatia vijana teknolojia stahiki kwa ajili ya kilimo chenye tija. Katika mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kuimarisha kambi ya vijana ya Mkongo – Rufiji kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji.

c. Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhia Nafaka

Katika mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kuimarisha hifadhi ya chakula nchini, kwa kuendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhi nafaka ya Songea na Mbozi na ukarabati wa sehemu mbalimbali nchini.

3.2.3 Viwanda

i. **Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga:** kuanza ujenzi wa mgodi, na kukamilisha usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha chuma - Liganga. Kwa upande wa Mchuchuma, kipaumbele kitawekwa katika ujenzi wa mgodi, kituo cha kuzalisha umeme, na ujenzi wa miundombinu. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha barabara ya Itoni - Mkiu - Mchuchuma - Liganga, ambapo eneo la Itoni Mkiu linatarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

ii. **Mradi wa Magadi Soda - Ziwa Natron, Arusha:** Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa magadi soda katika bonde la Engaruka na Ziwa Natron. Kipaumbele kitawekwa katika eneo la Engaruka ambapo tafiti za awali zimekamilika. Kazi zitakazofanyika ni kukamilisha tafiti za kitaalam (*Techno-economic study*),

kukamilisha mkataba na wabia kwa ajili ya kuendeleza mradi, na ujenzi wa miundombinu.

iii. **Kiwanda cha Viuadudu Kibaha, Pwani:** Kuendelea kusimamia uendeshaji wa kiwanda; na kufanya utafiti wa kutumia kiwanda hicho kwa ajili ya kutengeneza mbolea isiyokuwa na kemikali (biofertilizer);

iv. **Maeneo maalum ya uwekezaji:** maeneo ya kipaumbele ni pamoja na kukamilisha ulipaji fidia na kuanza ujenzi wa miundombinu katika eneo la Bagamoyo; na kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa *Master plan* kwa eneo la Tanga;

v. **Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini:** kuanza ujenzi wa kituo cha Biashara na Huduma Kurasini (Kurasini Trade and Logistics Hub).

3.2.4 Maendeleo ya Rasilimali Watu

i. Kuendelea kuimarisha uwezo wa kila Sekta kuandaa mipango ya maendeleo ya rasilimali watu na kuchambua mahitaji ya ujuzi;

ii. Kuendelea na upanuzi wa Vyuo Vikuu na vya ualimu hususan katika masomo ya Sayansi, katika vyuo vikuu vya Muhimbili (Kampasi ya Muhimbili na Mloganzila), SUA, Mzumbe, Ardhi na Dar es Salaam;

iii. Kuendelea kutoa mafunzo katika maeneo mahususi ya gesi na mafuta, chuma, urani, madini, umwagiliaji na maji;

iv. Kuendeleza elimu ya ufundi stadi kwa kuboresha mitaala na miundombinu katika vyuo vya ufundi, vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vya Maendeleo ya Jamii;

v. Kuendelea kuimarisha uwezo wa vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vya Maendeleo ya Jamii kwa kuendeleza na kuajiri wakufunzi wenye sifa;

vi. Kuendeleza ujenzi wa vyuo vya Ufundi Stadi katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa; na

vii. Kuendelea kuboresha mazingira ya ushiriki wa sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu na kutoa elimu katika sekta za elimu na afya.

3.2.5 Huduma za Utalii, Biashara na Fedha

A. Utalii

i. Kujenga na kuboresha vivutio vya utalii nchini;
ii. Kuongeza na kupanua vivutio pamoja na bidhaa za utalii;
iii. Kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya usafiri katika maeneo ya utalii; na
iv. Kuboresha ushiriki wa sekta binafsi hususan katika usafiri, hoteli na huduma nyingine za utalii.

B. Biashara na Masoko

i. **Uanzishaji wa Soko la Mazao na Bidhaa (Commodity Exchange Market):** Kuratibu ujenzi wa maghala makubwa yenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za mahindi katika mikoa sita ya nyanda za juu kusini ili kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa za soko hilo;
ii. **Uanzishwaji wa Tovuti ya Taifa ya Biashara (National Business Portal):** Kuweka mfumo wa kuwezesha utoaji wa Leseni na Ulipaji wa Ada za Leseni kufanyika kwa njia ya mtandao; na kuanzisha Mfumo wa Taarifa za masuala ya Biashara;
iii. **Kuendeleza Miundombinu ya Masoko:** Kuendelea na uratibu wa ujenzi wa masoko matano ambayo ni Kabanga - Ngara, Nkwenda - Nkenge, Murongo - Nkenge, Remagwe - Tarime, na Busoka - Kahama; na kuendelea na uratibu wa ujenzi wa masoko ya Segera na Makambako.

C. Huduma za Fedha

a. Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania – TADB

i. Kuendelea kuongeza mtaji wa benki;
ii. Kuanza utoaji wa mikopo kwa wananchi; na
iii. Kutafuta mikopo yenye riba ndogo hadi kufikia mtaji unaolingana na Dola za Kimarekani milioni 500.

b. Benki ya TIB

i. Kuanza rasmi kufanya kazi Disemba 2015 chini ya mfumo wa makampuni mawili yanayotegemeana (two tier structure). Ambapo TIB Development Bank itabakia na jukumu la kuangalia kwa

ukamilifu na umakini zaidi miradi mikubwa ya maendeleo na shughuli za kibiashara zitakuwa zimehamia kwenye kampuni tanzu ya TIB Corporate Finance Limited;

ii. Kutoa mikopo kwa miradi mikubwa ikiwemo ile ya miundombinu;

iii. Kushiriki kikamilifu katika sekta za kimkakati zikiwemo zile za mafuta, gesi na madini; na

iv. Kukopesha miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 300 kwa kutoa kipaumbele kwenye miradi ya viwanda vya usindikaji wa mazao na bidhaa mbali mbali, na pia kuendelea kusaidia miradi ya SMEs ili kuwawezesha wananchi.

c. Benki ya Wanawake Tanzania

i. Kuongeza bidhaa za benki katika soko hasa zile zisizotegemea mikopo kutoka asilimia 7% iliyopo sasa hadi kufikia 25%;

ii. Kuendelea kuongeza utoaji wa mikopo kwa watu binafsi, SACCOS, makampuni na vikundi mbalimbali vikiwamo vikundi maalum vya wajasiriamali wadogowadogo wanaojishughulisha na usindikaji wa chakula, kuuza chakula, Mitumba, Samaki na maduka madogo madogo;

iii. Kuendelea kupanua huduma sehemu mbalimbali zikiwemo Zanzibar, Mtwara, Katavi, Singida, Rukwa, Tabora, Arusha, Morogoro, Mara, Kagera, Lindi, Tanga, Kilimanjaro na Simiyu; na

iv. Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 250,000 ambapo asilimia 80 watakuwa ni wanawake.

3.3 Miradi Mingine Muhimu kwa Ukuaji wa Uchumi

3.3.1 Elimu na Mafunzo ya Ufundi

i. Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na mafunzo ya Stashahada ya Ualimu katika fani za masomo ya Sayansi;

ii. Kuendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) kupitia Mikakati ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Elimu kwa kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, kuinua mazingira ya kujifunzia na kufundishia kupitia upatikanaji wa vitabu, nyumba za walimu, maabara na maktaba, na kujenga mazingira rafiki ya utoaji wa elimu;

iii. Kuendelea kuimarisha miundombinu ya vyuo vikuu nchini, vyuo vya ufundi, vyuo vya ualimu, vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na vyuo vya Maendeleo ya Jamii;
iv. Kuboresha miundombinu na mazingira ya Taasisi za elimu kwa ajili ya kuongeza fursa za wanafunzi na walimu kujifunza na kufundisha hasa masomo ya Sayansi, hisabati na kingereza;
v. Kuendelea na ujenzi wa hospitali ya mafunzo katika Kampasi ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere – Butiama; na
vi. Kuboresha ukaguzi wa shule kwa kuvipatia vitendea kazi vituo vya kanda.

3.3.2 Afya na Ustawi na Jamii

i. Kuimarisha na kuongeza miundombinu na upatikanaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii katika: hospitali za rufaa za Kitaifa zikiwemo za Muhimbili, Moi, Mbeya, Bugando, KCMC na Ocean Road; na hospitali za kanda zenye kutibu magonjwa maalum za Mirembe na Kibong'oto;
ii. Kuimarisha upatikanaji wa vifaa tiba hususan katika hospitali za rufaa
iii. Kuimarisha ubora wa huduma za kinga na matibabu kwa kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuboresha sekta ya afya na programu za kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto;
iv. Kuimarisha na kuboresha taasisi za mafunzo ya afya kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa rasilimali watu katika sekta; na
v. Kuboresha mazingira ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza katika utoaji wa huduma za afya nchini.

3.3.3 Mifugo na Uvuvi

a. Mifugo

i. **Miundombinu ya maji na malisho:** Kuendelea na ujenzi wa malambo na majosho, pamoja na uchimbaji wa visima virefu; na kuendelea kutenga maeneo kwa ajili ya malisho katika wilaya mbalimbali nchini.
ii. **Vituo vya uhimilishaji:** Kuendelea kuimarisha vituo vya uhimilishaji vya Taifa vya Sao Hill, Iringa; na USA River, Arusha (NAIC-USA River); na kuimarisha vituo vya kanda.

iii. **Ujenzi wa Minada na Masoko:** kukamilisha ujenzi wa minada ya upili ya Longido na Kirumi na kukarabati minada katika maeneo mbalimbali.

iv. **Kuongeza thamani mazao ya mifugo:** Kuendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Ruvu yanayojengwa chini ya usimamizi ya kampuni ya Ranchi za Taifa - NARCO.

b. Uvuvi

i. **Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi:** kukamilisha upembuzi yakinifu na kuanza usanifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi.

ii. **Vituo vya Mafunzo na Tafiti za Uvuvi:** kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA); na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya vituo katika sehemu mbalimbali.

iii. **Huduma ya Uzalishaji wa Samaki:** kujenga vituo vya kuzalisha samaki; kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki wa maji ya bahari cha Mtwara; na kuendelea kuimarisha vituo vya Mbegani - Bagamoyo na Machui Tanga.

3.3.4 Madini

i. **Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini:** Kununua vifaa vya kisasa vya maabara za Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) na Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA); na kuwezesha uboreshaji wa Mfumo wa Utoaji Leseni; kuimarisha mtandao huo mikoani na kuanzisha *Data Recovery System* ya kutunza kumbukumbu za leseni za madini.

ii. **Uendelezaji wa Miundombinu ya Chuo cha Madini:** Kuendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya chuo cha madini ili kuboresha utoaji elimu kwa Watanzania walio wengi kuhusu utafiti, uchimbaji na usimamizi wa rasilimali za madini, gesi asilia na mafuta.

iii. **Ujenzi wa Ofisi za Kanda za Madini za Mikoa:** Kuendelea na ujenzi wa ofisi za madini za mikoa, ambapo kipaumbele kitakuwa kukamilisha ujenzi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mpanda na Mtwara.

iv. **Uendelezaji wa Miundombinu ya Wakala wa Jiolojia Tanzania**: Kuendelea kuimarisha Wakala wa Jiolojia kwa kuweka miundombinu ya kisasa ya maonesho na kuhifadhia sampuli katika

jumba moja la maonesho ya jiosayansi.

3.3.5 Usafiri wa Anga na Majini

a. Usafiri wa Anga

i. Kuendelea kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga ili kuongeza ufanisi wa viwanja vya ndege vya: Bukoba, Shinyanga, Mwanza, Kigoma, Mpanda, Tabora, Songwe, Mafia, Arusha, Musoma, Kilimanjaro, Julius Nyerere, na Mtwara.

ii. Kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji katika usafiri wa anga.

b. Usafiri wa Majini

i. Ununuzi wa meli mpya ambapo meli tatu (3) zitanunuliwa kupitia mkopo toka DANIDA; na

ii. Ukarabati wa meli za abiria na mizigo ambazo ni MV Umoja, MV Ukerewe na MV Sangara chini ya utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa, kukarabati Meli za MV Victoria, MV Liemba, MV Songea, na MV Iringa.

3.3.6 Hali ya Hewa

i. Kuimarisha miundombinu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kuongeza matumizi ya vifaa vya kisasa; na

ii. Kuimarisha uwezo wa Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kuongeza ufanisi.

3.3.7 Ardhi, Nyumba na Makazi

i. Kuimarisha utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi na utoaji wa hati miliki mijini na vijijini;

ii. Kuimarisha mipaka ya Kimataifa hususan kati ya Tanzania na Malawi, Kenya, Msumbiji, Burundi, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia;

iii. Kuanzisha Mfumo Unganishi wa Utunzaji na Upatikanaji wa taarifa na kumbukumbu za ardhi (Integrated Land Management Information Sytem - ILMIS); na

iv. Kuendelea na utekelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni na miji mingine; na

v. Kuimarisha shughuli za tafiti za vifaa vya ujenzi wa nyumba zenye

gharama nafuu.

3.3.8 Ushirikiano wa Kikanda

i. Kuimarisha vituo vya mtangamano wa kikanda;
ii. Kuimarisha mfumo wa utekelezaji wa soko la pamoja; na
iii. Kutekeleza Mpango Kamambe wa Kuendeleza Miundombinu kwa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

3.3.9 Misitu na Wanyamapori

i. **Wanyamapori:** Kutekeleza miradi ya Usimamizi Endelevu wa Maliasili (Sustainable Natural Resources Management in Tanzania); Mradi wa Kujenga Uwezo Katika Mapori ya Akiba na Vitengo vya Kupambana na Ujangili Nchini; na mradi wa Kilombero and Lower Rufiji Wetlands Ecosystem Management Project (KILORWEMP); na
ii. **Misitu:** Kutekeleza mradi wa kusaidia Utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Misitu na Ufugaji Nyuki II; na Mradi wa Kusaidia Uendelezaji wa Misitu Binafsi.

3.3.10 Utawala bora

i. Kuendelea na mpango maalum wa kujenga Ofisi za Mahakama Kuu katika mikoa ya Shinyanga, Dodoma na Bukoba. Aidha, Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama Kuu katika mikoa ya Kigoma, Mara, Lindi, Mtwara, Morogoro, Manyara na Singida. Miradi ya ujenzi wa Mahakama Kuu itaenda sambamba na uanzishwaji wa Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
ii. Kuimarisha na kuboresha miundombinu na vitendea kazi ya vyombo vya ulinzi na usalama;
iii. Kuboresha na kuongeza miundombinu ya Bunge kwa kukarabati majengo ya Ofisi, Dodoma na Dar es Salaam pamoja na kuendeleza ujenzi wa Ofisi za Wabunge majimboni;
iv. Kuendelea na mchakato wa kupata Katiba mpya;
v. Kuboresha na kuongeza miundombinu katika taasisi zinazohusika na masuala ya maadili na rushwa nchini;
vi. Kukamilisha uchaguzi mkuu;
vii. Kuendelea na mipango ya ujenzi wa Chuo cha Uongozi cha Taifa; na

viii. Kuendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kitaifa wa haki za binadamu.

3.3.11 Vitambulisho vya Taifa

i. Kuendelea na kazi ya usajili na utambuzi wa watu, utengenezaji na utoaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi katika mikoa na Wilaya kwa Tanzania Bara na Zanzibar;
ii. Kujenga na kuimarisha mfumo wa mawasiliano kati ya ofisi za usajili za wilaya na mikoa mbalimbali hapa nchini na makao makuu;
iii. Kuendeleza ujenzi wa kituo kikuu cha utunzaji wa kumbukumbu na uokozi wakati wa majanga katika jiji la Dar es Salaam; na
iv. Kuanzisha mfumo wa ubadilishaji wa taarifa na wadau muhimu katika sekta za Umma na Binafsi.

3.3.12 Kazi na Vijana

i. Kuendelea kutekeleza programu ya kukuza ajira kwa vijana itakayotekelezwa kwa miaka mitatu 2014/15-2016/17;
ii. Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili kuongeza uwezo wa mfuko kutoa mikopo na mafunzo ya kuwajengea vijana uwezo kupitia vikundi; na
iii. Kutekeleza tafiti za hali ya nguvukazi na hali ya utaalam nchini.

3.3.13 Mazingira

i. Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa athari za mazingira kwa miradi mikubwa ya viwanda na miundombinu; na
ii. Kuendeleza mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

SURA YA NNE

UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2015/16

4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16 ambao utagharamiwa na Serikali kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato, misaada, mikopo pamoja na ushiriki wa sekta binafsi.

4.2 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16)

Katika kugharamia mpango wa maendeleo wa miaka mitano, ilikadiriwa kuwa shilingi trilioni 8.9 zitahitajika kila mwaka, kati ya hizo shilingi trilioni 2.9 zitatokana na fedha za ndani katika bajeti ya Serikali na shilingi trilioni 6.0 zitatokana na uwekezaji wa sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Hivyo, katika kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, Serikali italazimika kutenga rasilimali za kutosha kila mwaka kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, msisistizo utakuwa ni kutumia rasilimali chache zilizopo katika kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi, ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

4.3 Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16

Serikali imeendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Katika mwaka 2013/14, zilitengwa jumla ya shilingi 5,644,988,950,000 ambapo fedha za ndani ni shilingi 2,952,920,112,000 na fedha za nje ni shilingi 2,692,068,838,000. Katika mwaka 2014/15, fedha zilizotengwa ni shilingi 5,699,088,062,800 ambapo fedha za ndani ni shilingi 3,682,821,139,000 na fedha za nje ni shilingi 2,016,266,923,800. Fedha zilizotolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2014/15 ni jumla ya shilingi 1,111,303,662,908 ambapo fedha za ndani ni shilingi 943,276,000,000 na fedha za nje ni shilingi 168,027,662,908. Katika mwaka 2015/16, fedha zinazokusudiwa kutengwa kugharamia miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 5,777 ambapo fedha za ndani shilingi bilioni 3,277 na fedha za nje ni shilingi bilioni 2,500.

4.4 Vyanzo vya Mapato ya Ndani

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kutumia vyanzo vya ndani vya mapato vilivyopo, vyanzo vipya vilivyopendekezwa katika maabara ya ukusanyaji wa mapato na kubuni vyanzo vingine kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Serikali itaendelea kukopa ndani ya nchi kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia sera ya kukopa ndani ya nchi isiyozidi asilimia moja ya Pato la Taifa.

4.5 Vyanzo vya Mapato ya Nje

Ili kuweza kuziba nakisi ya bajeti itakayotokana na vyanzo vya mapato ya ndani katika mwaka 2015/16, Serikali itaendelea kutumia vyanzo vya nje vya mapato hususan misaada na mikopo yenye masharti nafuu. Katika kufanikisha ugharamiaji wa miradi mikubwa ya miundombinu, Serikali itaendelea kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka kwa nchi marafiki na mashirika ya Kimataifa kwa kuzingatia ukomo wa uhimilivu wa deni la Taifa. Hali kadhalika, Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na nchi wahisani na mashirika ya kimataifa ili kusaidia utekelezaji wa Mpango.

4.6 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Serikali inaendelea kutumia mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan, miradi ya miundombinu. Serikali imekamilisha hatua mbalimbali katika eneo hili ikiwa pamoja na sera, sheria na kanuni zake. Elimu itaendelea kutolewa kwa wadau wa sekta binafsi ili washiriki kikamilifu katika uwekezaji kwa ubia na sekta ya umma.

4.7 Uwekezaji wa Sekta Binafsi

Serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi wa Taifa, hivyo kipaumbele kitawekwa katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia uwekezaji mkubwa wa sekta binafsi katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Aidha, sekta binafsi itaendelea kuhamasishwa kuendelea kuchangia shughuli za maendeleo ili kupunguza mzigo katika bajeti ya Serikali.

SURA YA TANO
UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MIRADI YA MAENDELEO

5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa muhtasari ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2013/14 na robo ya kwanza ya mwaka 2014/15 hususan miradi ya Kitaifa ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wake unaendana na malengo yaliyowekwa, kubaini changamoto na kushauri hatua za kuchukuliwa. Aidha, sura hii inaelezea utaratibu wa ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya maendeleo na ratiba ya uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16.

5.2 Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo

Katika kipindi cha mwaka 2013/14 na robo ya kwanza ya mwaka 2014/15, Tume ya Mipango ilifanya ufuatiliaji kwa baadhi ya miradi ya Kitaifa ya kimkakati katika sekta za kilimo, ujenzi, nishati, uchukuzi, maji, afya na viwanda kwa mikoa ya Dodoma, Tabora, Kigoma, Singida, Shinyanga, Mwanza, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Njombe, Ruvuma, Lindi, Tanga, Arusha, Mbeya Rukwa, Katavi na Mtwara. Miradi ya maendeleo iliyotembelewa kisekta ni kama ifuatavyo:-

i. **Sekta ya Usafirishaji -** Uboreshaji na Upanuzi wa **Viwanja vya Ndege** vya Tabora, Kigoma, Shinyanga, Iringa, Mtwara na Mwanza; ujenzi wa kiwanja cha ndege Songwe (Mbeya); Mpanda (Katavi); upanuzi wa **Bandari** za Kigoma, Mtwara na Mwanza; ujenzi wa Bandari ya Mwambani (Tanga); ujenzi wa Bandari ya Mbegani Bagamoyo (Pwani); na ujenzi wa reli ya Tanga - Arusha - Musoma (Tanga);

ii. **Sekta ya Ujenzi** - Ujenzi wa barabara ya Tabora – Kigoma, hususan vipande vya: Tabora - Ndono (km 42); Ndono - Urambo (km 52); Kaliua – Kazilambwa (km 56); Uvinza – Kidahwe (km 76.6), Kidahwe – Kigoma (km 36) na Daraja la Malagarasi pamoja na barabara zake (km 48); ujenzi wa barabara ya Kidatu - Ifakara (Morogoro); Ukarabati wa barabara ya Isaka – Ushirombo (km 132); Ukarabati wa barabara ya Ushirombo – Lusahunga (km 110); Ujenzi wa baraba ra Tunduma Sumbawanga (km 225); ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112); ujenzi wa daraja la Kilombero (mita 384) pamoja na

barabara zake km 9.142 (Morogoro); ujenzi wa daraja la Kigamboni mita 680 (Dar es Salaam); ujenzi wa daraja la Kavuu (Katavi); na Ofisi ya Madini Kanda ya Mtwara (Mtwara);

iii. **Sekta ya Nishati -** Ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara – Lindi – Dar es Salaam; ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa njia ya upepo wa MW 100 (Singida); ujenzi wa mtambo wa kusafisha gesi Madimba (Mtwara); ujenzi wa kV 220 za umeme Makambako - Songea (Njombe); Mradi wa kusambaza umeme vijijini - Mbeya na Rukwa; na ujenzi wa mtambo wa kufua umeme MW 150 Kinyerezi (Dar es Salaam);

iv. **Sekta ya Viwanda** - ujenzi wa Eneo Maalum la Uwekezaji, Kigoma – SEZ; SEZ Bagamoyo (Pwani); kiwanda cha saruji cha MEIS na Lee construction (Lindi) na EPZ Mtwara; ujenzi wa kiwanda cha saruji cha Dangote (Mtwara); kiwanda cha Viuadudu (Pwani); Kituo cha Biashara na Uwekezaji - Kurasini (Dar es Salaam); Magadi-Soda - (Manyara);

v. **Sekta ya Maji -** ujenzi wa bomba kuu la kusafirisha maji kutoka ziwa Victoria hadi Shinyanga – Kahama – Nzega – Igunga – Tabora; Mradi wa Vijiji Kumi (Iringa, Mbeya na Katavi); Ruvu Juu na Ruvu Chini (Pwani);

vi. **Sekta ya Kilimo** – Mradi wa Umwagialiaji, Mbarali (Mbeya); mradi wa ujenzi wa ghala la nafaka, Mbozi (Mbeya); Kiwanda cha mbolea cha Minjingu (Manyara); ujenzi wa ghala la chakula Songea (Ruvuma); Programu ya Maendeleo ya Vijana iliyopo Wilaya ya Igunga (Tabora); Programu ya Maendeleo ya Vijana katika Wilaya ya Sikonge (Tabora); na Kambi ya Vijana ya kilimo – Mkongo;

vii. **Sekta ya Mifugo na Uvuvi -** ujenzi wa Machinjio ya Ruvu (Pwani); Taasisi ya Utafiti wa uzalishaji na uendelezaji wa mifugo Mpwapwa (Dodoma); na ujenzi wa Kituo cha kutotoleshea na kukuzia vifaranga vya samaki uliopo Katonga-Kigoma;

viii. **Sekta ya Afya -** ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Singida, Mbeya na Mtwara; Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Tiba Mloganzila;

ix. **Sekta ya Ardhi -** Ujenzi wa Mji Mpya Kigamboni,

x. **Sekta ya Elimu -** Chuo Kikuu cha Ufundi, Mbeya; na

xi. **Taasisi za Fedha -** Benki ya Rasilimali, tawi la Mwanza.

5.3 Tathmini ya Miradi ya Maendeleo

Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo inaonesha kuwa:-

i. Miradi mingi ilikuwa nyuma ya mpango-kazi kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa fedha, taratibu za manunuzi na madeni ya miaka iliyopita;
ii. Taratibu za tathmini na ulipaji wa fidia kwa wakati imekuwa ni changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya miradi. Aidha, taratibu za muda mrefu za kupata hati miliki za maeneo ya miradi kumesababisha wananchi kuvamia maeneo ya mradi na kudai kulipwa fidia mara kwa mara;
iii. Ufuatiliaji na tathmini ya miradi kutokuwa endelevu kwa baadhi ya miradi; na
iv. Miundombinu na huduma wezeshi hususan barabara, maji na umeme imechangia kwa kiasi kikubwa uchelewaji wa utekelezaji wa miradi.

5.4 Utekelezaji wa Mpango-kazi

5.4.1 Mafanikio

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Julai 2013 hadi Juni 2014, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni:

i. Utaratibu wa kujikita katika miradi michache hususan kuwa katika mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa umewezesha kuwa na matokeo mazuri katika hatua mbalimbali za utekelezaji;
ii. Mwitikio wa uwasilishaji wa taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa miradi ya maendeleo umekuwa mzuri. Hii imesaidia kujua hatua za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuangalia namna ya kuondokana na changamoto zinapojitokeza; na
iii. Mwitikio wa kuandaa maandiko ya miradi umekuwa wa kuridhisha. Hii imesaidia kuwa na picha halisi ya miradi ya maendeleo kwa kuwa taarifa za msingi za mradi kama vile faida za mradi, mahitaji ya rasilimali fedha na ukomo wa mradi.

5.4.2 Changamoto

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kulikuwa na changamoto mbalimbali zilizojitokeza. Changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Miradi mingi ipo nyuma ya ratiba kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa fedha na madeni ya miaka iliyopita;
ii. Ushiriki mdogo wa Sekta binafsi katika kutekeleza uwekezaji unaozingatia vipaumbele vya Mpango wa Mwaka;
iii. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kujirudiarudia kwa baadhi ya miradi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupitwa na wakati na masharti ya wafadhili; na
iv. Upatikanaji wa ardhi iliyopimwa kwa ajili ya kuwezesha mradi kutekelezwa.

5.4.3 Hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na Changamoto

Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza. Hatua zinazopendekezwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

i. Kuendelea na juhudi za kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani (ya kodi na yasiyo ya kodi); uchambuzi wa misamaha ya kodi na kupanua wigo wa kodi;
ii. Serikali imeanzisha mfuko wa kuwezesha ubia baina ya sekta ya umma na binafsi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
iii. Wizara na Taasisi kuzingatia mipango kazi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na
iv. Utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo ya uwekezaji.

5.5 Utekelezaji wa Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa

Utekelezaji wa Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa umekuwa ukiendelea katika mikondo mikuu miwili inayotegemeana. Mkondo wa kwanza ni kujenga na kuimarisha mfumo utakaohakikisha kuwa matokeo tarajiwa katika mikakati ya maendeleo yanapatikana, na mkondo wa pili ukiwa ni kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi iliyoaininishwa katika maeneo makuu sita yaliyohusika na awamu ya kwanza ya uchambuzi wa Kimaabara (Uchukuzi, Kilimo, Elimu, Maji, nishati ya umeme, na ukusanyaji wa mapato). Aidha, awamu ya pili imefanyia uchambuzi maeneo ya kuboresha mazingira ya Biashara na uwekezaji nchini na awamu ya tatu ya kuboresha huduma za afya.

Utekelezaji wa miradi ya Matokeo Makubwa Sasa ulianza baada ya uchambuzi wa maabara kukamilika ambapo Mawaziri wa wizara sita zinazotekeleza mfumo huo waliingia mikataba ya Utendaji na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Makatibu Wakuu katika wizara hizo pamoja na watendaji wao, wakuu wa mikoa yote, Makatibu Tawala wa mikoa, pamoja na watendaji wao, wote waliingia mikataba hiyo ya utendaji kazi ili kufikia malengo yaliyowekwa. Kuanzia Julai 2013 utekelezaji huu umekuwa ukifuatiliwa na kusimamiwa kwa njia ya zifuatazo:

i. Kuundwa kwa Vitengo Maalum vya Ufuatiliaji katika wizara (Ministerial Delivery Unit – MDU) ambavyo huandaa taarifa za utekelezaji za kila wiki na kila mwezi na kuziwasilisha Ofisi ya Rais, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo;
ii. Kuundwa na kuanza kazi kwa Kamati Maalum za kusimamia utekelezaji katika eneo kuu la Matokeo (NKRA Steering Committees) katika wizara zinazotekeleza miradi ya Matokeo Makubwa Sasa. Kamati hizi zimeundwa na wawakilishi wa wadau muhimu katika kuhakikisha miradi inatekelezwa na matokeo tarajiwa yanapatikana. Kamati hizi zinaongozwa na Mawaziri husika na zinakutana mara moja kila mwezi kujadili mwenendo wa utekelezaji, hususan, kutatua vikwazo na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji; na
iii. Kuundwa na kuanza kazi kwa Baraza la Kusimamia Mageuzi na Utekelezaji (Transformation and Delivery Council – TDC). Baraza hili ambalo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndilo lenye mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa.

5.6 Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo 2015/16

Wizara/Taasisi zinazohusika moja kwa moja katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo zitahitajika kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo katika maeneo yao na kuandaa taarifa za kila robo mwaka na mwaka. Taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo zitawasilishwa Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itaratibu ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika ngazi za Sekretariati za Mikoa na

Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa upande wa miradi ya kimkakati ya kitaifa, jukumu la ufuatiliaji na tathmini litakuwa ni la Tume ya Mipango na Wizara/Taasisi. Aidha, Ofisi ya Rais, Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi – PDB itaendelea kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi iliyo chini ya programu ya Matokeo Makubwa Sasa.

5.7 Muhtasari wa Ratiba ya Utekelezaji

Utaratibu na ratiba ya maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16 utakaowasilishwa Bungeni Juni, 2015 ni kama ifuatavyo:

Jedwali Na 6.1: Ratiba ya Uandaaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2015/16

Na.	Shughuli	Muda	Mamlaka Husika
1	Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa 2015/16	Oktoba, 2014	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango
2	Kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa 2015/16 katika Kamati ya Bunge ya Bajeti	Novemba, 2014	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango
3	Bunge kupokea, kujadili na kutoa maoni ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16	Novemba, 2014	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango
4	Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16	Novemba, 2014 – Aprili, 2015	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali
5	Uchambuzi wa Bajeti ya maendeleo kwa mwaka 2015/16	Januari – Februari 2015	a) Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Wizara ya

Na.	Shughuli	Muda	Mamlaka Husika
			Fedha, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali b) Wizara ya Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, Sekretariati za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa
6	Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 kuwasilishwa na kujadiliwa katika katika Kamati ya Bunge ya kudumu ya Bajeti	Machi, 2015	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango
7	Bunge kupokea Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 kujadili na kuidhinisha	Juni, 2015	Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango

SURA YA SITA

MKAKATI WA KUKABILIANA NA VIASHIRIA HATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO

6.1 Utangulizi

Kulingana na taarifa za Shirika la Fedha Duniani (IMF, 2014), hali ya uchumi wa Dunia inatarajiwa kuimarika mwaka 2014 na 2015. Ingawa kuna dalili hizo za kuimarika bado kuna vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2015/16. Hali hii itailazimu Serikali kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na viashiria hivyo hatarishi ili Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2015/16 utekelezwe kwa ufanisi.

6.2 Viashiria hatarishi vya Utekelezaji wa Mpango

Vihatarishi ambavyo vinaweza kupunguza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2015/16 ni pamoja na:

i. **Ugharamiaji wa Mpango 2015/16:** Dalili zinaonesha kuwa madeni, riba na adhabu kwa miradi ya ujenzi na barabara zitaongezeka na hali hiyo inaweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

ii. **Upatikanaji wa Fedha za Misaada na Mikopo:** Miradi ya maendeleo imekuwa ikitegemea misaada na mikopo kutoka katika mashirika ya kifedha na nchi washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wake. Upatikanaji wa mikopo na majadiliano kuchukua muda mrefu ikiwemo masharti magumu; na

iii. **Mabadiliko ya Tabianchi:** Uharibifu wa mazingira hususan unaosababishwa na ukataji ovyo wa miti na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika matumizi ya rasilimali asili yasiyo endelevu, imesababisha kuwepo kwa mvua nyingi zisizokuwa na msimu, ukame na mafuriko na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii. Hali hii, inatarajiwa kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2015/16.

6.3 Hatua za Kukabiliana na Viashiria Hatarishi vya Utekelezaji wa Mpango

Katika kukabiliana na viashiria hatarishi vya utekekelezaji wa Mpango wa

Maendeleo mwaka 2015/16, Serikali italazimika kuchukua hatua zifuatazo:-

i. Kuongeza mapato ya ndani kwa kuwianisha mapato na matumizi pamoja na kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi, na kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwenye miradi ya maendeleo zinalindwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa;
ii. Serikali itaendelea kufanya mazungumzo na wahisani kuhusu fedha za misaada na mikopo ili iweze kupatikana kama ilivyokusudiwa na kwa masharti nafuu; na
iii. Kujenga uelewa wa wananchi juu ya utunzaji wa mazingira na kujenga uwezo wa kitaasisi katika kukabiliana na majanga (preparedness and surveillance).

BIG RESULTS NOW PROJECTS AND PROGRAMMES 2013/14 – 2015/16

1. AGRICULTURE

1.1 Commercial farms pilot deal
1.2 Smallholder rice irrigation schemes
1.3 Small holder collective marketing system

2. EDUCATION

2.1 STEP Primary – Teacher training
2.2 STEP Primary – Enrichment Classes
2.3 STEP Secondary – Teacher training
2.4 STEP Secondary – Enrichment Classes
2.5 3R assessment
2.6 3R teacher training
2.7 Official school ranking
2.8 School incentive Scheme
2.9 School improvement toolkit
2.10 Capitation grants
2.11 Basic facility construction
2.12 Teacher Motivation

3. ENERGY

3.1 Gas infrastructure
3.2 Sustainable water management
3.3 Transmission system upgrade
3.4 Distribution system upgrade
3.5 Electrification
3.6 Demand management and energy efficiency
3.7 EPP and IPP dispatch and fuel purchase mechanism
3.8 Kinyerezi I
3.9 Kinyerezi II
3.10 Iringa-Singida-Shinyanga (400 kV; 657 km. (Backbone Transmission Investment Project-BTIP

3.11 Dar – Chalinze- Tanga- Arusha (400 kV; 682 km)
3.12 Dar – Morogoro-Dodoma: 400 kV; 431 km + Morogoro Substation Upgrade to 400/220 kV)
3.13 Singida- Arusha: 400 kV; 315 km
3.14 Somanga-kinyerezi: 220 kV; 203 km
3.15 Makambako –Songea 220 kV; 300 km
3.16 Bulyanhulu- Geita 220 kV; 55 km+ Rural Electrification for 15 Villages in Geita District
3.17 Nyakanazi – Kigoma – Mbeya 220 kV transmission line: 1148 km
3.18 Enhancing TANESCO's financial viability and accountability

4. WATER

4.1 Construction of new, extension and rehabilitation of existing water point
4.2 Operation and maintenance of existing good water points
4.3 Enabler to facilitate projects and O&M

5. TRANSPORT

Port

5.1 Transform Dar es Salaam port operational process
5.2 Implementation of port communication system
5.3 Removal/ relocation of unutilized facilities to improve port layout
5.4 Maximize port spatial efficiency by improving road access and traffic
5.5 Upgrading existing rail access infrastructure at the port
5.6 Upgrading port infrastructure to increase handling capacity (short term)
5.7 Modernization of port infrastructure as building block (long term)
5.8 Lake port upgrading and workforce enhancement
5.9 Strengthening institutional administration

Rail

5.10 Establishment institutional set-up;
5.11 Rehabilitation of railway infrastructure (track, bridges, station building);

5.12 Improve availability and reliability of rolling stock;
5.13 Create business plan and reestablish financial and cargo-monitoring;
5.14 Adapt organizational set-up for RAHCO and TRL; and
5.15 Improve maintenance procedure.

Road

5.16 Infrastructure enhancement of critical roads;
5.17 Building supporting routes;
5.18 Port and Border posts services and Facilities;
5.19 Reducing non tariff barriers;
5.20 Continuous road maintenance; and
5.21 Improve and enforce road safety standards.

6. RESOURCE MOBILIZATION

6.1 Review excise duty rates to advalorem at regional levels and expanding list of excisable items;
6.2 Adjust the fuel levy to account for inflation;
6.3 Introduce a withholding income tax on commercial imports;
6.4 Introduce an Education Investment Levy;
6.5 Reducing the stock and flow of tax exemptions;
6.6 Enhancing Customs valuation; and
6.7 Introducing an expenditure cap at 2013/14 levels.

KIAMBATANISHO II

MAPENDEKEZO YA MAABARA YA KUBORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA NA UWEKEZAJI, 2015/16

NA.	ENEO	HATUA ZILIZOPENDEKEZWA
1.	Kuoanisha mfumo wa kisheria na kitaasisi	• Sheria ya Usajili wa Biashara iliyoboreshwa (Business Activities Registration Act (BARA) (2007) ichukue nafasi ya sheria ya Leseni za Biashara Business Licensing Act (1972) na Business Name (Registration) Cap 213; • Kutengeneza mfumo wa masijala unaojumuisha taarifa kutoka katika taasisi mbalimbali zinazohusika na usajili wa biashara mfano TRA, NSSF, BRELA; • Kurahisisha mchakato wa kuanzisha biashara ; • Kuondoa vibali na leseni zenye mwingiliano na zinazojirudia; na • Kurahisisha mchakato wa sheria na kanuni za biashara (Ukaguzi na adhabu)
2.	Upatikanaji wa ardhi na usalama katika umilikishaji	• Kuboresha mfumo wa taarifa za ardhi nchini sanjari na maboresho yaliyofanyika katika ramani ya kijiografia, kufikia Disemba 2016; • Kumaliza mrundikano wa madai/kesi za ardhi zilizopo katika mabaraza ya ardhi ya wilaya na kuyapatia mabaraza hayo vitendea kazi stahiki ifikapo

NA.	ENEO	HATUA ZILIZOPENDEKEZWA
		Disemba 2016; • Kupanua wigo wa upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo ya miji na vijiji kufikia Disemba 2016; na • Kufanya Kampeni kubwa ya kusambaza elimu kuhusu utunzaji wa ardhi na mafanikio katika uwekezaji.
3.	Usimamizi na Uratibu wa shughuli za Biashara, Utitiri wa Kodi, tozo na ada	• Kufanya uchambuzi wa athari za kanuni kwa Wizara 5 na Halmashauri 20 ifikapo mwishoni mwa 2014; • Kuanzisha kituo kitakachosimamia uratibu wa shughuli za biashara jijini Dar es Salaam ifikapo mwishoni mwa 2014; • Kuondoa/kupunguza kero kumi (10) katika kodi, ada na tozo ifikapo Disemba, 2015; • Kuanza Kukusanya kodi ya isiyopungua shilingi bilioni 50 kwa mwaka kutoka kwa wachimbaji wasio rasmi hadi kufikia mwisho wa mwaka 2014; na • Kuharakisha zoezi la ukadiriaji na urejeshwaji wa kodi ndani ya siku 30 baada ya maombi kuwasilishwa
4.	Kuzuia na Kupambana na Rushwa	• Kuanza kutekeleza programu ya kuwatangaza hadharani watu waliokutwa na hatia ya makosa ya rushwa ifikapo mwisho wa mwaka 2014;

NA.	ENEO	HATUA ZILIZOPENDEKEZWA
		• Ahadi ya uadilifu (integrity pledge) kufikia Aprili 2014; • Kesi tano (5) kubwa zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuchunguzwa, kushitakiwa, na kutolewa hukumu ifikapo Disemba, 2014; na • Asilimia 35 ya kesi za rushwa zinazoendelea kutolewa maamuzi ifikapo mwishoni mwa 2014 • Kutekeleza utaratibu wa manunuzi kwa mfumo wa kielektroniki;
5.	Sheria na stadi za kazi	• Marekebisho sheria ya ELRA ya mwaka 2004 ifikapo 2015; • Kuimarisha Taasisi zinazoshughulikia ajira nchini (Mahakama ya Kazi; Ofisi za kazi); • Usimamizi wa elimu ya ufundi kuwa chini ya chombo kimoja ifikapo 2015 • Kuboresha maadili, mtazamo na uwajibikaji katika kazi; na • Kupunguza kiwango cha wafanyakazi wenye ujuzi wa chini kufikia asilimia 70 ifikapo 2016
6.	Usimamizi wa Mikataba na Utawala wa Sheria	• Kuondoa mrundikano wa kesi katika mahakama zote; • Mashauri kusikilizwa katika muda uliopangwa katika ngazi zote za mahakama ifikapo 2015 • Kupunguza muda wa kusikiliza shauri kufikia siku 65; • Asilimia 10 ya mashauri ya Serikali kumalizwa kwa njia ya usuluhishi;

NA.	ENEO	HATUA ZILIZOPENDEKEZWA
		na • Kuzindua jukwaa la kielekroniki la kutolea malalamiko kuhusu mahakama

KIAMBATANISHO III

MAPENDEKEZO YA MAABARA YA KUBORESHA HUDUMA ZA AFYA, 2015/16

NA.	ENEO	MKAKATI
1.	Mgawanyo wa Watumishi wa Sekta Afya	• Kutoa kipaumbele kwa mikoa yenye upungufu mkubwa wa watumishi wakati wa kuidhinisha vibali vya ajira; • Kupata watumishi wenye ujuzi kwa kushirikisha sekta ya umma na binafsi; • Kusambaza upya watumishi kutoka sehemu zenye watumishi wengi kwenda maeneo yenye upungufu; • Kutekeleza sera ya kushinikizwa (bonding) kwa watumishi wa sekta ya afya; • Kuhakikisha Halmashauri zinatekeleza wajibu wake kuajiri na kubakiza watumishi katika maeneo yao; • Kuhakikisha uwepo wa mkakati wa kuajiri na kubakiza watumishi katika Halmashauri; • Kuhakikisha uwepo wa mkakati wa kuajiri na kubakiza watumishi katika Halmashauri na • Kuimarisha maendeleo ya ujuzi wa usimamizi wa rasilimali Watu katika Halmashauri.
2.	Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba	• Kuboresha mfumo wa kitaasisi wa usambazaji dawa na vifaa tiba kwa kuboresha mtaji wa Idara ya Bohari ya Dawa; • Kuongeza mapato yanayokusanywa katika vituo vya kutolewa huduma za afya na kuhakikisha kuwa asilimia 50

NA.	ENEO	MKAKATI
		inatumika katika ununuzi wa dawa na vifaa tiba; • Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kusambaza dawa na vifaa tiba; • Kuboresha mfumo wa 5S-Kaizen katika vituo vya afya ili kuimarisha utunzaji kumbukumbu za dawa na vifaa tiba; • Kuongeza matumizi ya simu za mkononi kwa ajili ya utunzaji wa kumbukumbu za dawa na vifaa tiba; • Kuimarisha mifumo ya uwajibikaji na utawala katika usimamizi wa dawa na vifaa vituoni; na • Kushirikisha jamii kusimamia uwajibikaji na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba vituoni.
3.	Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto	• Kujenga uwezo wa zahanati na vituo vya afya vilivyochaguliwa katika mikoa mitano ya Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Kigoma, kutoa huduma ya msingi ya dharura ya afya ya uzazi na mtoto, ikiwa ni pamoja na upasuaji kwa mama wajawazito; • Kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu huduma za afya ya uzazi na mtoto ili kuboresha ufahamu, mtazamo, mienendo chanya na kuongeza matumizi yake kwa jamii; na • Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na mtoto zinazotolewa na wahudumu wa afya katika jamii kupitia mtandao wa simu za mkononi.
4.	Kupima ufanisi wa Utoaji wa Huduma za	• Kuanzisha Mfumo wa Kitaifa wa Kupima Ubora wa Vituo na Huduma (Star Rating System);

NA.	ENEO	MKAKATI
	Afya	• Kutekeleza dhana ya ugatuzi wa madaraka kwa lengo la kuongeza uwezo wa vituo vya afya kusimamia ukusanyaji wa mapato na kuvipatia uwezo na uwajibikaji wa kuboresha huduma za afya; • Kuongeza ushiriki na uwajibikaji wa wananchi katika kuainisha na kutekeleza vipaumbele vya afya; na • Kuwa na viwango na mikataba ya kupima ufanisi wa watumishi wa afya ili kuongeza uwajibikaji na kutoa huduma bora.